# HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Kamati ya Amani na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, Sheikh Alhad Mussa Salum, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kongamano la Siku ya Maridhiano linalotarajiwa kufanyika Dodoma Machi 3, mwaka huu na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan. Kushoto ni Mjumbe wa Kamati hiyo, Christosiler Kalata. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Lema atua kwa kishindo, apata mapokezi makubwa

**Na Waandishi Wetu,** SIHA/ ARUSHA

NI kishindo. Ndivyo ilivyokuwa kwa mamia ya wafuasi wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutoka mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, walivyojitokeza jana kumlaki aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, aliyerejea nchini baada ya miaka miwili kuishi uhamishoni nchini Canada.

Wafuasi hao wakiwa kwenye magari, watembea kwa miguu na waendesha pikipiki walikusanyika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro wakiwa na bendera za chama hicho na zingine kwenye miti kwa ajili ya kumlaki kiongozi huyo ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA.

Wafuasi hao walifika uwanjani hapo kuanzia alfajiri na kabla ya Lema kuwasili na wengine walisimama barabarani eneo la makutano ya barabara ya KIA na barabara kuu ya Arusha/Moshi wakiusubiri msafara wake. Walikuwa wakitamka maneno 'Mama (Rais Samia Suluhu Hassan) hana baya na mtu jamani, Lema wetu karudi!

Maneno hayo yalisikika saa chache baada ya msafara wa Rais Samia kupita eneo hilo kwenda Arusha huku wananchi na wafuasi wakiupungia na kushangilia.

Lema alitua nchini kwa kutumia ndege Shirika la Ndege la Ethiopia saa 6:30 mchana na kupokewa na familia, viongozi mbalimbali wa CHADEMA, mwanasheria wake, Prof. George Wajackoya ambaye ni raia na mwanasiasa wa Kenya.

Pilikapilika za hapa na pale za wananchi waliokuwa wamebeba matawi ya miti, waendesha bodaboda, bajaji, magari madogo, Toyota Hiace na Toyota Coaster, zilikuwa ni shamrashamra ya aina yake. Magari hayo yalifunga barabara, umbali wa kilomita sita kutoka yalipo makutano ya barabara kuu ya Arusha/Moshi, kuingia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Magari hayo yaliwanyima utulivu polisi na kuweka nguvu kubwa kuzuia ajali au rabsha za hapa na pale.

Katika mapokezi hayo, polisi walipata wakati mgumu zaidi kuyazuia makundi ya waendesha bodaboda yaliyokuwa yakiendesha vyombo hivyo vya moto kwa kukimbiza kuanzia Maji ya Chai, Kikatiti, King'ori hadi KIA.

Wakati wote vijana hao walikuwa wakijaribu kuendesha kwa kasi, kutembea kwa gurudumu la nyuma na kunyanyua pikipiki juu ili kuamsha hisia na kuchochea hamasa ya watu kufuatilia msafara huo.

**ANGAMIZA CHAWA**

Wakati anazindua tawi hilo, Lema alisema: "Nimekuja na 'slogan' mpya ya angamiza chawa wote. Nimekuja na dawa ya kuangamiza chawa wote, niacheni nianze kuwapulizia dawa."

**MBOWE, NIDHAMU MUHIMU**

Akizungumza katika mkutano huo, Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA, Freeman Mbowe, alisema nyenzo ya CHADEMA ni nidhamu, hivyo anawasihi wananchi hasa wanachama wake kuwa na nidhamu.

Alisema yeye pamoja na majukumu mengi ya chama, bado ana jukumu la kumpokea na kumpeleka Lema kwa wazazi wake.

"Ndugu yangu Godbless Lema, nitaendelea na maridhiano ya Katiba mpya na Rais (Samia Suluhu Hassan). Nakukabidhi Kanda ya Kaskazini, piga kazi usiku na mchana kuhakikisha Katiba mpya inapatikana na wananchi wanarudisha tabasamu.

"Lema akiwa ughaibuni, alikuwa akifuatilia kwa karibu siasa za Tanzania, hivyo anajua kila kilichokuwa kinaendelea nchini Tanzania. Nakupongeza sana, Profesa George Wajackoyah kwa namna ulivyompatia ofisi nchini Kenya, akawa anaendelea na mambo ya chama wakiwa Kenya."


DANISH REFUGEE COUNCIL

**TANGAZO LA ZABUNI**

**SHIRIKA LA KUHUDUMIA WAKIMBIZI LA DANISHI LINATARAJIA KUINGIA MKATABA WA HUDUMA ZA BIMA YA AFYA KWA BINADAMU.**

HIVYO SHIRIKA LA DANISHI LINATANGAZA ZABUNI TAJWA HAPO JUU NA WAZABUNI WAFUATE MAELEKEZO YAFUATAYO.

- USIFUTE KWENYE BEI
- USITUMIE WINO WA MAJI KUSAHIHISHA UNAPOFANYA KOSA.TUMIA KARATASI MPYA
- USIBADILISHE KARATASI ZA ZABUNI KWENDA KWENYE MFUMO WORD/EXCEL,
- ZINGATIA SEHEMU ZA KUSAINI NA KUGONGA MUHURI AMBAZO NI LAZIMA
- USISAHAU KUAMBATANISHA NYARAKA ZINAZOHITAJIKA KAMA VILE KIAMBATISHO A.1, KIAMBATISHO A.2, CHETI CHA KUKUBALI TUZO YA ZABUNI NA KANDARASI, WASIFU WA MUUZAJI NA FOMU YA USAJILI, HALI YA MKATABA WA JUMLA WA DRC, MAELEZO YA KAMPUNI, KANUNI YA MWENENDO WA WASAMBAZAJI WA DRC BAADA YA KUMALIZA SEHEMU ZOTE KAMILI, SAINI, GONGA MUHURI, WEKA TAREHE.

KWAHIYO SHIRIKA LA DANISHI LILILOPO KIBONDO LINAWAALIKA WAZABUNI KULETA BEI ZAO.
NYARAKA ZA KUJAZIA BEI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI ZA DANISHI KIBONDO KUANZIA TAREHE 02.03.2023 HADI TAREHE 15.03.2023 SIKU ZA KAZI SAA 2:00 ASUBUHI MPAKA SAA 10:30 JIONI. TUNAPATIKANA BARABARA YA IRC KIBONDO.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA **+255621897518 au BARUA PEPE alan.mvano@drc.ngo**
ZABUNI ZITAFUNGULIWA HADHARANI TAREHE **17.03.2023 SAA 4:00 ASUBUHI** OFISI ZA DANISHI KIBONDO NA KAMATI YA KUFUNGUA ZABUNI.

**UNAWEZA KURUDISHA ZABUNI KUPITIA RFQ.TZA@DRC.NGO AU KULETA MOJAKWA MOJA OFISINI VINGINEVYO NI BATILI.**


## Meya ashtushwa kushamiri biashara ya ukahaba Dar

**Na Halfani Chusi**

MSTAHIKI Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge, ameiomba serikali kuingilia kati ongezeko la wanawake wanaouza miili yao maarufu 'changudoa' kwenye madanguro, akisema sasa imekuwa kufuru.

Songoro aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipofanya ziara ya kushtukiza kwenye danguro la Mwananyamala Minazini, Kata ya Makumbusho, kujionea biashara hiyo ilivyoshika kasi maeneo hayo.

Alisema, ameyaona madanguro zaidi ya 150, ambayo 'madada poa' wamepanga katika nyumba na wamegawa vyumba vipande vidogo vidogo kwa ajili ya kufanyia biashara hiyo.

Kutokana na hali hiyo, kiongozi huyo aliwataka wenye nyumba waliopangisha watu hao kufika ofisini kwake, kujieleza sababu ya kukubali nyumba zao kutumika kwa ukahaba.

"Hatua ya kwanza tunataka kuwatambua wamiliki wenye hizi nyumba, hawa wote wamepangishwa hakuna mwenye nyumba ina maana mwenye nyumba amegeuza nyumba yake kuwa sehemu ya machangudoa kufanyia biashara haramu.

"Kama mlivyoona kwenye ile nyumba namba 108 inaonekana wakati inatengenezwa ilikuwa ina vyumba sita, lakini sasa ina vyumba zaidi ya 20 vidogo vidogo ambavyo wao wanaviita 'passport size' kinawekwa mlango mbele na nyuma.

"Hawa waliokimbia hapa wamepangishwa na wanalipa kodi kubwa, ndiyo maana nikasema jambo hili linahitaji msaada wa serikali kuu nikisema tuvunje hizi nyumba hapa nitaonekana nimeingilia haki za binadamu na uhuru wa watu, lakini hakuna uhuru usio na mipaka," alisema.

Alisema sheria lazima ifuatwe na serikali haiwezi kuendelea kuona jamii inaangamia kwa sababu ya watu wachache wanaoshindwa kujishughulisha na kubadili ukahaba kuwa sehemu ya maisha yao ya kila siku.

Alifafanua kuwa ni vigumu kupambana na maradhi ya maambukizi kama Ukimwi na mengine yatokanayo na ngono, ikiwa mtu mmoja anahudumia watu wengi kwa mara moja.

Pia aliwaasa wakazi wa maeneo hayo, kutoa taarifa kila wanapoona mambo hayo yanajirudia huku akiwataka viongozi wa serikali ya mtaa kukemea vitendo hivyo.

"Inawezekana kuna mambo yanafanyika kinyume na utaratibu kwa maana zipo taarifa zisizo rasmi kwamba wanachanga fedha halafu wanapeleka kwenye mamlaka ambazo zilipaswa kuzuia vitendo hivyo jambo ambalo haliwezi kukubalika.

"Kuna watoto wanasoma, na wao wakiona wataona hakuna haja ya kusoma watashawishika kuiga na baadaye kupoteza malengo yao, kwa hiyo nikimaliza kuzungumza hapa mwenye nyumba akajisalimishe mwenyewe kwenye ofisi ya mkuu wa wilaya," alikemea.

Pia alisema kuna madanguro mengine Msasani na Uwanja wa Fisi Manzese na tamko hilo linahusu madanguro yote.

Diwani wa Kata ya Makumbusho, Mohamed Ali, alisema kwenye kupambana na madhila hayo hatua aliyochukua ni kupeleka taarifa Manispaaa ya Kinondoni, huku akishukuru kwa kutii na kuchukua hatua kuanza kuteketeza biashara hiyo.

**WAKAZI WAFUNGUKA**

Peter Chikila, mkazi wa eneo hilo alisema licha ya kufanya 'biashara', bado hugeuka kuwa kichaka cha kufanyia uhalifu kwa kuwaibia wateja wanaopenda kupata huduma hiyo.

"Mtaa huu na wa nyuma yake bado ni vichaka vya kulea wahalifu, unapatana naye kwa Sh. 2,000 au 3,000 ukiingia ndani akiona hela pia anaweza kukuibia, ndoa za watu zinavunjika kupitia hawa wanawake wa kwenye madanguro," alilalamika.

Mohamed Abdalah, mkazi wa eneo hilo alisema biashara hiyo sio nzuri maeneo hayo akidai inawaharibu watoto kisaikolojia.

"Athari ni kubwa tutakuwa tunaambukiza vizazi na vizazi kwa kuwa watakua wanaona kitu cha kawaida hii ni njia ya wanafunzi kwenda shule na pia hapa ni sehemu iliyopo karibu na Ofisi ya Mtendaji Kata, sasa hatujui kama kuna chochote wanapewa mpaka wanakaa kimya.

Mama Ntilie maeneo hayo, Maria Manguva, aliwashauri kinadada wanaofanya biashara hiyo, kuachana nayo na kufanya shughuli za ujasiriamali huku akiitaka serikali kuweka mkazo kukomesha biashara hiyo.

Awali, kwenye kikao cha baraza la madiwani kilichofanyika wiki iliyopita, baadhi ya madiwani walishauri kuhalalishwa kwa jambo hilo ili wahusika wapewe leseni kutokana na ugumu wa kuidhibiti.

# Polepole: Nyasa, Ileje kuwa Kariakoo ndogo

**Na Romana Mallya**

BALOZI wa Tanzania nchini Malawi, Humphrey Polepole, amesema wamependekeza Wilaya ya Nyasa na Ileje mkoani Ruvuma na Songwe ziwe maeneo maalum ya kiuchumi kwa kujengwa Kariakoo ndogo itakayowezesha wafanyabiashara wa nchi hiyo na zilizopakana kwenda kununua bidhaa eneo hilo.

Akihojiwa jana asubuhi katika Kipindi cha Kumepambazuka cha Radio One, Balozi Polepole aliwataka wawekezaji kuchangamkia fursa hiyo.

"Ile Kariakoo inakuwa kubwa kama Dubai na sisi tunakwenda kutengeneza Kariakoo ndogo Nyasa na Ileje haya ndiyo mapendekezo," alisisitiza.

Balozi Polepole alisema badala ya wafanyabiashara wa nchi hizo kufunga safari mpaka Kariakoo, Dar es Salaam, watapata urahisi wa kupata bidhaa hizo kupitia Kariakoo hiyo iliyopendekezwa.

Alitaja kipaumbele kingine kuwa ni kufufua na kuipatia chapuo ushoroba wa Mtwara, kwa kujenga Bandari ya Mbambabay na Bandari Mtwara ili ziweze kufanya kazi.

Alisema tayari hilo walishalisema serikalini na maelekezo yameshatolewa kwa Mamlaka ya Bandari ya Tanzania (TPA) na ujenzi wake unatarajia kuanza mwezi huu.

Alisema ili wawashawishi Wamalawi ni lazima wawaonyeshe ule ushoroba unafanyakazi, ikiwamo miundombinu ya barabara.

"Mamlaka ya Bandari inatakiwa kujenga bandari na ninasisitiza kwamba Bandari ya Mbambabay ijengwe haraka, kitu cha umuhimu ni kufanya uamuzi kwa wakati kwa kuwa wakichelewa, sitafurahi kuona kazi niliyotumwa na mamlaka ya nchi inakwamishwa kwa sababu ya mtu fulani anachelewa kutekeleza jukumu lake."

Balozi Polepole alisema Bandari ya Mbambabay ndio mpango mzima kwa kuwa itaufungua Mkoa wa Ruvuma wilaya za Nyasa na Mbinga na mikoa ya Mbeya na Mtwara.

Aidha, alisema mwezi huu hadi Mei, watakuwa na Watanzania wengi wanaokwenda Malawi kununua mahindi, maharage, karanga nyekundu na mbaazi.

"Kazi yetu ni kuhakikisha tunajenga mazingira rafiki wakija wasitapeliwe wakutane na wauzaji halali, wasikinzane na sheria na jambo kubwa tulilolifanya kwa sasa unapokuja Malawi usitembee na fedha, hii ni hatari.

"Pili, usibadilishe fedha katika njia zisizo rasmi, tumezungumza na benki kubwa mojawapo Tanzania na kuiunganisha na benki nyingine kubwa inayofanya kazi Malawi ambapo wameingia ubia na mazungumzo yapo sehemu nzuri, anayekwenda kununua mazao Malawi ataweka fedha benki."

Kuhusu afya alisema ni moja ya vipaumbele vya mabalozi walivyojiwekea kwa kusogeza huduma bobezi kwenye matibabu ya mifupa, figo na moyo kwa kuunganisha Hospitali ya Benjamin Mkapa na Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) na Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Alisema wameshaiuanganisha JKCI na Hospitali ya Queen Elizabeth nchini humo ili kufanya kazi pamoja ya huduma bobezi, utafiti na wiki ya pili ndani ya mwezi huu (Machi), madaktari bingwa wa taasisi hiyo watakwenda Malawi kufanya vipimo na mjadala.

**KATAA WAHUNI**

Alipoulizwa kuhusu kampeni yake aliyoianzisha akiwa nchini Tanzania ya 'Kataa wahuni' alisema ni ya kudumu kwa kuwa wahuni sio watu wazuri wana hujumu vitu mbalimbali.

"Wahuni ni watu wabaya na wanaohujumu mustakabali wa nchi yetu, na mimi nina ushahidi nikisema kitu kwa kujiamini wewe chukua, nina ushahidi wa wahuni nilishawahi kuulizwa, wahuni bado wapo?

# RC aonya wagonjwa kufanyishwa kazi kabla ya kupatiwa matibabu

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, amewaonya baadhi ya watumishi wa Idara ya Afya mkoani humo kuwafanyisha usafi wagonjwa wanaokwenda kupata matibabu na kuwapa huduma baada ya kumaliza kazi.

Onyo alilitoa jana alipokuwa katika zahanati ya Kijiji cha Nambogo, Manispaa ya Sumbawanga alipokuwa kwenye ziara ya kutatua kero mbalimbali za wakazi wa kijiji hicho.

Mmoja wa wakazi hao, Maria Katasha, alimlalamikia Mkuu wa Mkoa kuwa katika zahanati hiyo kuwapo na mtindo mgonjwa anapofika hupewa vifaa vya kufanyia usafi na eneo la kusafisha, akimaliza ndipo apate matibabu.

"Mkuu wa mkoa sisi tunashangaa hapa hospitali yetu tunakuja na mgonjwa au anakuja mtu ni mgonjwa akifika anapewa jembe apalilie na kufanya usafi maeneo ya hospitali, akimaliza ndipo anapewa matibabu," alilalamika.

"Unakuta sisi wengine ni kinamama unakesha usiku kucha na mtoto analia kwa kuumwa hulali, ukifika hapa hospitali badala ya kutibiwa unapewa eneo ufanye kwanza usafi... kitendo hiki kinatuudhi sana kwakweli tunaomba uwaeleze waache tabia hiyo labda wewe watakuelewa."

Mkuu huyo alimuuliza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Sebastian Siwale, ambaye alikiri kupokea malalamiko hayo na kusema kuwa tayari amekwishaanza kuchukua hatua kwa kufanya uchunguzi.

Alikemea kitendo hicho na kumwagiza Ofisa Utumishi kuwaondoa watumishi hao katika kituo hicho kwa kuwa hataki vituo vya afya na zahanati za mkoa huo kuwa na watumishi wanaofanya mambo kinyume na taratibu.

Alisema, baadhi ya watumishi wanaharibu nia njema ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuboresha huduma katika sekta ya afya na kamwe hatawavumilia watu hao katika mkoa wake.







## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala Iugala, Nala Segu kukamilisha malipo ya viwanja hivyo mapema.

Mwananchi au taasisi itakayoshindwa kulipia kiwanja hadi kufikia tarehe 25 Machi, 2023 atambue kuwa kiwanja hicho kitauzwa kwa mteja mwingine ili kuboresha huduma katika Halmashauri bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**

Joseph C. Mafuru
**MKURUGENZI WA JIJI**
**DODOMA**

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
S.L.P. 1249,
DODOMA

217303602

# Mwinyi: Atakayeficha chakula kushtakiwa uhujumu uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewaonya wafanyabiashara watakaohodhi chakula na kupandisha bei za bidhaa hasa kipindi cha mwezi wa Ramadhani na kwamba serikali yake haitosita kuwachukulia hatua kali.

Alisema hakuna sababu ya bei za vyakula kupanda kwa sababu hali ya chakula nchini ipo vizuri.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwandishi wa gazeti hili kuhusu mfumuko wa bei, wakati wa kikao chake kati yake na waandishi wa habari kilichofanyika juzi, Ikulu Zanzibar. Alisema serikali itawafungulia kesi za uhujukumu uchumi wafanyabiashara watakaobainika kuficha vyakula kwa lengo la kuwapandishia bei wananchi.

"Tunategemea mwezi wa Ramadhani hakutakuwa na uhaba wa mchele, unga, sukari wala mafuta ya kula kwa sababu bidhaa hizi zipo za kutosha," alisema.

Alisema kipindi kifupi kilichopita baada ya mkutano wake na wafanyabiashara wa vyakula kufuatia kupanda kwa bei za bidhaa za vyakula, ghafla vyakula vilienea nchi nzima.

"Kuhodhi vyakula ili vipande bei ni uhujumu uchumi, atakayeficha vyakula tutamshtaki kwa kosa la uhujumu uchumi, tumetaarifiwa, mchele upo, sukari ipo, ngano ipo na mafuta yapo," alisisitiza.

Alisema mfumuko wa bei, sio tatizo la serikali bali linachangiwa na sababu mbalimbali za kidunia hasa ikizingatiwa kuwa Zanzibar inaingiza mchele kutoka Pakistani ambako kumekumbwa na mafuriko, inaagiza ngano kutoka Ukraine ambako nako kumekumbwa na vita baina yao na Urusi hali iliyosababisha bei za vyakula kupanda. Alisema pia Zanzibar inategemea vyakula kutoka Tanzania Bara, ambako kwa baadhi ya mikoa inayozalisha vyakula ilikumbwa na janga la ukame. Aidha, alisema kuilaumu serikali kwa mfumuko wa bei sio jambo sahihi kwa sababu serikali inayopandisha bei za bidhaa.

Alisema kwenye bei ya vyakula kosa sio la serikali yake na anawashangaa wanaofanya hivyo kwa sababu kuilaumu serikali sio jambo sahihi. Dk. Mwinyi alisema serikali itaendelea kusimamia mfumuko wa bei, ili kuwapa unafuu wananchi, lakini unafuu huo hautakuwa kama ilivyo kwa miaka ya nyuma kwa sababu bidhaa zimepanda bei tokea huko zinakotoka.

Baadhi ya wananchi wa Zanzibar waliozungumza na Nipashe kuhusu hotuba ya Rais, walisema ni jambo jema na lenye kuwapa matumaini ya kumudu gharama za chakula hasa katika mwezi wa Ramadhani, mahitaji yanapoongezeka.

Haji Juma, mkazi wa Kijiji cha Kisakasaka, alisema baadhi ya wafanyabiashara huufanya mwezi wa Ramadhani kuwa wa biashara na hupandisha bei za vyakula na kuwaumiza wananchi wanyonge.

"Tunawaomba viongozi wamsaidie Rais wetu, wasikae ofisini waende sokoni na madukani kuangalia bei za bidhaa kwa sababu sisi wanyonge ndio tunaosumbuka," alisema Asha Hamad, mkazi wa Magomeni Unguja.

Aidha, alisema wananchi wanye kipato cha chini wanashindwa kumudu gharama za chakula na wengi wao wanakula mlo mmoja kwa siku.

"Mwezi wa Ramadhani tunashinda kutwa bila ya kula kitu chochote hivyo inapofika muda wa kula tunahitaji kupata chakula kizuri sasa kama bei za bidhaa zitakua juu tutalala na njaa."

## Chongolo: Tanzania haijazidiwa na mikopo

**Na Waandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema Tanzania haina mzigo wa mikopo kama baadhi ya watu wanavyopiga kelele.

Alibainisha hayo jana akiwa ameambatana na sekretarieti ya chama hicho, wilayani Iramba ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya kuangalia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho kwa mwaka 2020-2025 katika Mkoa wa Singida.

"Wapo jamaa wanapiga kelele kuwa Tanzania inakopa sana na wanakaza nyuso na shingo zao kutaka kuonesha nchi hii inakopa sana, niwaambie tu katika nchi za Afrika Mashariki, nchi ambayo haina mzigo wa mikopo kuliko zingine zote ni Tanzania," alisema. "Hicho wanachopigia kelele kwamba tunakopa hakuna duniani nchi ambayo haikopi niwape mfano mimi nina fursa ya kusema hivi karibuni huko duniani Marekani ilikopa kwa China, ilienda kuomba kukopa ili mambo yao yatatuliwe."

"Watu wote mnajua Marekani ndio dunia nyingine, nendeni mkaangalie mjiridhishe mimi ni kiongozi mkuu wa chama siwezi kudanganya nimetaja kwa jina kwa sababu ni ukweli, hapa kuna mtu hajui kukopa? Kuna mtu amewahi kufa kwa kukopa?" Alihoji. Alisema mtu yeyote asiyetaka maendeleo hutengeneza mazingira ya kujifunga kama kisiwa na kusisitiza nchi zote zinakopa.

"Mwaka 1961 wakati tunapata uhuru hakukuwa na senti moja wakoloni walihakikisha wameswaga kila kitu, lakini Mwalimu (Hayati Julius Nyerere), baada ya kukabidhiwa nchi ndani ya miezi miwili alianza kukopa ili kuanza kujenga nchi inayojitegemea," alisema.


## NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED, JADA INVESTMENT LIMITED, MAJEMBA COMPANY LIMITED na NZIGE AUCTION MART. Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MMILIKI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MOHAMED RAMADHAN FOTA | 1.MOHAMED RAMADHAN FOTA<br>2. HAWA HUSSEN MBARUKU | 1. NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA<br>2. NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA. | 1KINYEREZI BONYOKWA, WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM<br>2. KINYEREZI BONYOKWA, WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 18/03/2023, SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JADA INVESTMENT LIMITED |
| 2 | ROSE EMMANUEL GADAU | ROSE EMMANUEL GADAU | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | MLOGANZILA, WILAYA YA UBUNGO, DAR ES SALAAM | 25/03/2023, SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JADA INVESTMENT LIMITED |
| 3 | FORTUNATUS S. JOHN MANGWELA | EMMY J. SWEBE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI No: TMK 015779 | KICHEMCHEM MBAGALA KUU WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 25/03/2023, SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LTD |
| 4 | JULIUS MWAKALONGE | MARTHA WILLFRED MITULLA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI No:ILA008855 | UKONGA, MAZIZINI WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 18/03/2023, SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LTD |
| 5 | RAMADHANI BAKARI HAMISI | HALIMA MUSA MWINJUMA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA WA MERA KATA YA SOMANGILA | MWERA , WILAYA YA KIGAMBONI DAR ES SALAAM | 15/04/2023, SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LTD |
| 6 | JUDEX CONTRACTORS LTD | SALMON RAPHEL MANG'IRA ODUNGA | NYUMBA YENYE HATI No.53663 | MBWENI MALINDI WILAYA KINONDONI- DAR ES SALAAM | 29/4/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART& GENERAL BROKERS LTD |
| 7 | ALEDONGI COMPANY | RAHEL E MTAYOBA | KIWANJA CHENYE LESENI NAMBA DSMT1010635 | SALASALA, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 29/4/2023, SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKERS LTD |
| 8 | UMABAMABA | UMABAMABA | BAJAJI, REGISTARTION No.MC 320 CVU, MAKE - TVS | BUNJU, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 17/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELE | MAJEMBA COMPANY LIMITED |
| 9 | UMABAMABA | UMABAMABA | BAJAJI,REGISTRATION No.MC 374 CVU, MAKE - TVS | BUNJU, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 17/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MAJEMBA COMPANY LIMITED |
| 10 | UMABAMABA | UMABAMABA | BAJAJI, REGISTRATION No.MC 727 CVU, MAKE - TVS | BUNJU, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 17/03/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MAJEMBA COMPANY LIMITED |
| 11 | UMABAMABA | UMABAMABA | BAJAJI, REGISTRATION No.MC 661 DBV, MAKE - SINORAY | BUNJU, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 17/03/2023,4:OO ASUBUHI NAKUENDELEA | MAJEMBA COMPANY LIMITED |
| 12 | UMABAMABA | UMABAMABA | BAJAJI, REGISTRATION No.MC 610 CWG, MAKE - SINORAY | BUNJU, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 17/03/2023: SAA 6: 00 MCHANA NAKUENDELEA | MAJEMBA COMPANY LIMITED |
| 13 | SIMON JOHN MBILANGA | SIMON JOHN MBILANGA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI No.TMK042730 | KICHANGANI, AZIMIO, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 18/03/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | NZIGE AUCTION MART |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED | JADA INVESTMENT LIMITED | MAJEMBA COMPANY LIMITED | NZIGE AUCTION MART |
|---|---|---|---|
| P. O. Box 62163<br>Dar es Salaam<br>Tel: 0658100737, 0757276263<br>Email: amazauctionma@gmail.com | P. O. Box 69098<br>Dar es Salaam<br>Tel: 0788493699, 0768085727<br>Email: | P.O BOX 10031<br>ARUSHA<br>Tel: 0785 934 209, 0754 929 299<br>Email: majembacompany20@gmail.com | P.O. BOX45492<br>DAR ES SALAAM<br>Tel: 0789606444, 0787337045, 0719668211<br>Email: |

217305102

## HABARI KITAIFA

# Ukatili wachochea kasi maambukizi VVU

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imekiri kuwa kukosekana kwa usawa, uwapo wa mila zilizopitwa na wakati, ubaguzi, kutengwa na unyanyapaa vimekuwa vikichangia kwa kiasi kikubwa kasi ya maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU).

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akitoa hotuba ya ufunguzi wa Siku ya Kimataifa ya Kupinga Unyanyapaa na Ubaguzi, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene.

"Tukumbuke pia kuwa kama ambavyo takwimu zetu zinavyoonyesha tunapoongelea usawa wa kijinsia, mila hatarishi na ukatili ni wanawake na wasichana ndio wahanga (waathirika) wakubwa," alisema Senyamule.

Alisema kutokana na kukataliwa au kutengwa na familia, marafiki na jamii nzima, watu wengi wanaoishi na VVU au ambao wako kwenye hatari ya kupata maambukizi, wameachwa wakiwa wamekwama na wakiwa wapweke wasioweza kupata huduma wanazohitaji.

"Pia unyanyapaa na ubaguzi kwenye makundi ya wanaojidunga dawa za kulevya umewasababishia wengi miongoni mwao kupata maambukizi ya VVU.

Kuna uhusiano mkubwa kati ya maambukizi ya VVU na usawa wa kijinsia," alisisitiza.

Senyamule alisema maambukizi zaidi ya VVU miongoni mwa wanawake na wasichana yanasababishwa na kutokuwepo kwa usawa katika mahusiano ya kijinsia na ukatili wa kijinsia.

Pia alisema ukatili wa kijinsia ni kichocheo cha maambukizi na madhara yatokanayo na VVU.

"Baadhi ya wanawake na wasichana wamepata maambukizi ya VVU kutokana na ukatili wa kingono, wanawake wenye VVU wako katika hatari ya ukatili hasa baada ya kuweka wazi hali zao za maambukizi," alisema.

Kadhalika, alisema tabia, mila na desturi hatarishi vimepelekea kukosekana kwa usawa wa kijinsia na ukatili wa kijinsia Tanzania, hali hiyo inachochea na kuongeza kiwango cha maambukizi na baadhi ya matukio yanayosababisha kuambukizwa na kusambaza VVU, kati ya wanawake na wasichana.

Vilevile alisema wanawake wameathirika zaidi kutokana na hali ya kutokuwepo kwa usawa katika uhusiano wa kijinsia na majukumu ya kijinsia pamoja na kutopewa fursa ya kufanya uamuzi.

Hata hivyo alisema serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Baraza la Taifa la Wanaoishi na Virusi vya Ukiwmi (NACOPHAO) wamefanikisha kuhamasisha watu wanaoishi na VVU kujiunga kwenye konga ambapo hushirikiana pamoja kujikwamua kiuchumi, kupeana taarifa mbalimbali, na hata kuhudumiana.

Senyamule alisema wengi wanaishi maisha ya kawaida na kushiriki shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

Alitoa rai kwa majukwaa ya viongozi wa dini kutumika kuelimisha jamii kuhusu madhara ya unyanyapaa na ubaguzi pamoja na kujenga mifumo thabiti ya upendo na kusaidiana.

Pia alisisitiza kuwa ni vyema pia makanisa na misikiti iwe na sehemu maalum ya kutoa ushauri kwa waumini wao.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
02.03.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumamosi tarehe 04-03-2023** kampuni ya **Spedag Interfreight Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Mzenga kuelekea Dar -Es-Salaam kupitia Mlandizi** gari hiyo ina namba ya usajili: **NRB 97300 / NRB 54202**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 23.00** |
| **Upana** | - | **mita 4.30** |
| **Kimo** | - | **mita 4.60** |

3. Njia itakayotumika: **Mzenga, hadi Dar -Es-Salaam kupitia Mlandizi** gari itasafiri muda wa mchana tu (***Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***




Mbunge wa Morogoro Mjini, Dk. Abdulaziz Abood (wa nne kushoto), akikabidhi msaada wa tani saba za mifuko ya saruji kwa uongozi wa Shule ya Sekondari ya Kitungwa, Kata ya Kingolwira, Manispaa ya Morogoro jana, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya kidato cha tano na sita. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# DC apiga marufuku watuhumiwa ubakaji kupewa barua za dhamana

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MKUU wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okashi, amepiga marufuku watendaji wa vijiji na kata wilayani humo kutoa barua za dhamana kwa watuhumiwa wanaofikishwa kituo cha polisi kwa vitendo vya ubakaji au udhalilishaji.

Okashi alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo kilichofanyika kujadili utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema katika wilaya hiyo bado kuna tatizo kubwa la vitendo vya ukatili vinavyofanywa kwa watoto jambo ambalo kama halitakemewa litahatarisha ustawi.

Alikemea tabia ya baadhi ya viongozi wanaopewa taarifa za watoto kufanyiwa ukatili na kushawishi mzazi kutofikisha tukio hilo kituo cha polisi na badala yake wakae meza moja na mtuhumiwa kumaliza kesi hizo. Okashi alivielekeza vyombo vya ulinzi na usalama kufuatilia kwa kina matukio ya ubakaji na udhalilishaji yanayoripotiwa na hatua zinazochukuliwa.

Wakati huo huo, aliomba jamii kushirikiana kulea watoto kwa maadili ili kujenga jamii ya watu wanaochukia mambo yanayoenda kinyume na maadili na kukomesha uhalifu kwenye jamii na mambo yasiyofaa. Katika baraza hilo Mkuu huyo wa wilaya pia amegawa pikipiki sita kwa watendaji kata zilizotolewa na Serikali Kuu.


TANGAZO MAALUM

KIWANJA KINAUZWA

KAOLE-BAGAMOYO



BEACH PLOT

KIWANJA KINAMILIKIWA KIHALALI

AREA:1.238HA ≈ 3.059 ACRES ≈ 12,380 SQUARE METERS

TITTLE NO: 11422PWN | L.O.NO. 179016 | L.D.NO. BAG/6514

TAREHE YA USAJILI: 06.08.2022 | TERM: 33 YEARS

KWA MAWASILIANO PIGA SIMU:

0713646776 / 0718 799957

0713 939377

217304802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uhuru wa wanahabari katika kuibua mambo uwe na mipaka

**WAZIRI** wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, juzi alifanya ziara katika vyombo vya habari vya IPP ikiwa ni mwendelezo wa kutembelea na kujifunza mambo mbalimbali katika tasnia ya habari.

Licha ya kutembelea vyombo hivyo, Waziri Nape amekuwa akitoa matamko mbalimbali kuhusu ufanyaji kazi katika tasnia ya habari, kikubwa zaidi akisisitiza weledi kwa wanahabari katika kila wanachokifanya.

Akiwa katika ziara yake juzi IPP Media, Waziri Nape aliwataka wanahabari nchini kuacha woga katika kuandika habari ili kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan katika kufichua madudu yaliyoko katika serikali na taasisi zake. Kwa kufanya hivyo, kwa mujibu wa Nape, kutawezesha kuibua maovu mbalimbali yakiwamo ubadhirifu, rushwa na utekelezaji hafifu wa miradi ya maendeleo unaofanywa na baadhi ya viongozi na watendaji.

Pia kupitia kalamu za wanahabari, pindi maovu yatakapoibuliwa, taasisi zilizopewa mamlaka ya kufanya uchunguzi ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa pamoja na zile za ulinzi na usalama na vyombo vya sheria, zitachukua hatua dhidi ya wale watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Kubwa zaidi alilolisema Waziri Nape katika ziara yake hiyo juzi, ni waandishi wa habari waache kuwa na hofu wanapofichua madudu hayo kwa kuhofia kuchukuliwa hatua ikiwamo vyombo vyao kufungiwa. Aliwahakikishia wanahabari kuwa hakuna atakayechukuliwa hatua kwa kuwa serikali imeamua kuwa mlezi na si kuadhibu vyombo hivyo huku akisisitiza kuwa zama za hofu zimekwisha.

Ni dhahiri kwamba serikali ya sasa chini ya Rais Samia, imedhamiria kurejesha uhuru wa vyombo vya habari ambao kwa takriban miaka saba iliyopita ulikuwa katika arijojo. Hiyo inatokana na sheria ngumu zilizotungwa ili kuminya na kukandamiza uhuru wa habari pamoja na ule wa kukusanyika na kujieleza.

Pamoja na kauli hiyo ya Waziri kwamba waandishi wa habari waache hofu katika kuandika habari zinazolenga kuisaidia serikali kubaini madudu kama rushwa, wizi na ubadhirifu pamoja na uchepushaji wa fedha za maendeleo, ni vyema weledi na misingi ya taaluma vikatawala katika kutekeleza jukumu hilo la utoaji habari.


Kuna msemo kwamba hakuna uhuru usio na mipaka. Vivyo hivyo kwa wanahabari katika utekelezaji wa majukumu yao, wanapaswa kuheshimu sheria za nchi na kufuata misingi ya taaluma na weledi. Wanapaswa kuandika ukweli kuhusu yale wanayoyafichua ndani ya jamii na taasisi za serikali pamoja na wale wanaodaiwa kuhusika na mambo hayo, kupewa nafasi ya kusikilizwa.

Vyombo vya habari ni mhimili wa nne wa dola kutokana na nafasi viliyopewa katika jukumu kubwa la kuuhabarisha, kudunisha na hata kuuonya umma juu ya yale yanayotendeka siku hadi siku.

Kutokana na umuhimu huo, vinapaswa kufanya mambo hayo kwa misingi ya utawala bora. Kwa maneno mengine, havipaswi kumkomoa au kumwonea mtu kwa kumbambikia kashfa na mambo ambayo hayana ukweli ndani yake.

Ni imani kwamba kwa kufanya hivyo na kwa kufuata misingi ya taaluma na weledi, vyombo vya habari vinaweza kupata heshima ya hali ya juu na hata kusaidia kupunguza au kutatua matatizo yanayoikabili jamii na pia kulinda rasilimali za nchi ambazo ziko hatarini kuporwa na watu wachache.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# 'Chimba dawa' inavyowadhalilisha wanawake wakiwa safarini kwa basi

**NENO** chimba dawa sio geni kwa abiria wote wanaosafiri kwa mabasi kwenda mikoa mbalimbali nchini.

Unapoanza safari, utasikia matangazo kutoka katika basi yakisema kutakuwa na dakika tano za kuchimba dawa, kutakuwa pia na dakika 10 za kupata chakula mahali fulani.

Huo sio utaratibu mgeni, umekuwapo miaka mingi, ikiendana na mabadiliko ya barabarani, aina ya magari na hata mazingira ya huko tunakokuwa safarini, lakini kuchimba dawa kumedumu kuwapo palepale.

Ni katika hatua hiyo ya maendeleo, nako tunashuhudia kuwapo mabasi mengi yanayotoa huduma kwenda katika mikoa mbalimbali, baadhi yamejikamilisha kimuundo zaidi, ikiendana na wakati ikiwamo huduma za chakula na vyoo. Naam! Ni sehemu ya maendeleo, sibishani nayo hata kidogo

Pia, kuna mabasi mengine yenyewe bado yanasimama katika zama zile za huko nyuma. Hapo nikisafiri, nashuhudia baadhi ya mabasi, nyendo zao zimekosa ustaarabu katika utaratibu huo wa kuchimba dawa.

Unakuta wanasimamisha gari zao pembeni ya barabara na kuwaambia abiria kwamba wanawapa dakika tano za tendo hilo la kuchimba dawa.

Hasa ndiko penye mzizi wa swali langu, hivyo kweli dakika chache, zina sifa ya kuwezesha kinamama wote walio katika hali tofauti, wakachimba dawa na kuendelea na safari kwa amani?

Nikiwa mwanamama, nasema hicho hakiwezekani nikiwa na ushuhuda wa uhalisia njiani, abiria zaidi ya 60 wanashuka na kuchimba dawa, hata kuwahi warudi ndani ya gari wamekamilisha kilichowatoa nje ya gari.

Mabasi hayo hayo yanawadhalilisha sana wanawake katika kuchimba dawa. Yaani wanafanya hivyo hadharani, wakishuhudiwa jirani na kinababa walioko nao katika mchakato huo.

Gari mnasimamisha hakuna hata uwezekano wa kujificha mwanamke ajistiri na tendo hilo la kisaikolojia kwa mwanadamu, tena magari mengine unakuta watu wanachimba dawa huku magari yakipita na kuona kinachoendelea.

Huo ni udhalilishaji sana na ni maeneo ambayo mamlaka za kiserikali kama vile LATRA, inayosimamia usafiri zichukue hatua, kuona namna mwanamke anabaki kuheshimiwa katika masuala ya uchimbaji dawa safarini na faragha ya lazima inayomgusa.

Niseme, kuna mbadala wa namna nyingi, mfano stendi zenye vyoo vya kulipia. Mkishusha abiria kuna tatizo gani penye huduma kama hizo, hadi mkabaki kuwapeleka mahali pasipofaa, ndio wakachimbe dawa?

Suala la kuchimba dawa lizingatie sana haki za wanawake na binadamu kwa jumla na hilo ni sehemu ya jukumu la msingi hata kwa LATRA. Kuwaacha watu wanachimba dawa hovyo hovyo barabarani, mnafika mbali ikiwamo uchafuzi wa mazingira.

Katika dharura hizo, mtu atajisaidia hata haja kubwa na kuiacha hapo, je nani hapo wa kulaumiwa katika athari hizo za kimazingira na tujiulize, walio wenyeji wa mahali hapo, kimsingi tunawaachia nini?

Hata tukihamia kwennye hoja za zile dakika 10 za kupata chakula tena basi zingine zinatoa dakika tano, kwanza ukifika katika maeneo hayo kupata chakula unakuta magari, mengine yapo na yameshusha abiria nao wanakimbilia chakula na safari ya chooni inaanza.

Vilevile, katika baadhi ya safari, kuna abiria wanashindwa kutimiza vitu vyote kwa pamoja, kwa kuhofia kuachwa na gari. Hivyo wenye mabasi mnatakiwa kuwajali abiria wenu kwa kuanza kuwapeleka maeneo sahihi kwa ajili ya kuchimba dawa?.

Iwapo, suala la kuchimba dawa litaendelea kiholela, kutasababisha uchafu wa mazingira na hata magonjwa ya kuambukiza. Hasa pale inaponyesha mvua watu kukanyaga vinyesi vya wanaochimba dawa hovyo hovyo.

# Mahakama yatoa hati kukamatwa walimu wanaodaiwa kuvujisha mitihani

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imetoa hati ya kuwakamata walimu wanne walioshtakiwa kwa kuvujisha Mtihani wa Taifa wa darasa la saba mwaka 2022 kwa kukiuka masharti ya dhamana.

Amri ya kutolewa kwa hati hiyo imetolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Pamela Mazengo, wakati kesi hiyo ilipotajwa na washtakiwa hao kutoonekana mahakamani bila kutoa taarifa.

Wakili wa Serikali, Faraji Nguka alidai kesi hiyo ilikuwa inatajwa, lakini washtakiwa wanne hawakuwapo mahakamani.

Aliwataja washtakiwa hao kuwa ni mwalimu Jacob Adagi, Joel Ngome, Lloyd Mpande na Leonard Odongo.

Awali, Wakili Nguka alidai mahakamani kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika.

Washtakiwa walipoitwa majina hawakuwapo na hawakutoa taarifa ndipo mahakama ilipotoa hati za kuwakamata kwa kukiuka masharti ya dhamana.

Hakimu Mazengo aliutaka upande wa mashtaka kuharakisha upelelezi wa kesi hiyo.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Johnson Ondieka, Patrick Chawawa, Theresia Chitanda, Elinami Sarakikya, Joyce Nkomola, Docras Muro na Alcherous Malinzi.

Inadaiwa kuwa kati ya Oktoba 2 hadi 12 mwaka 2022, jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao walisambaza mtihani huo kupitia mtandao wa kijamii wa Whatsapp na Telegram na kusababisha kuvuja kwa watu ambao hawakuwa na mamlaka ya kuusimamia.

Inadaiwa kwamba katika tarehe hizo Mkoa wa Dar es Salaam, mshtakiwa Malinzi alitengeneza nyaraka za uongo kuonesha kama Mtihani wa Taifa wa Darasa la saba wa somo la Uraia, na somo la Maadili na Maarifa ya Jamii akionesha ni halali iliyotolewa na Baraza la Taifa la Mitihani wakati akijua si kweli.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Herman Kasekende (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, katika mkutano wa kuwasilisha ripoti ya utunzaji mazingira hapa nchini unaofanywa na benki hiyo. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania, Masanja Kadogosa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watoto wawili wateketea kwa moto wakiwa ndani

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WATOTO wawili wa familia moja katika Kijiji cha Kitandu Shinga, Moshi mkoani Kilimanjaro, wamefariki dunia baada ya nyumba waliyokuwamo kuteketea kwa moto.

Watoto hao, Greyson Kimaro na Bright Kimaro, wenye umri chini ya miaka mitano walikuwa ndani ya nyumba hiyo wakati moto unaanza.

Mmoja wa mashuhuda wa ajali hiyo, Lightness Wiliam, alisema moto huo ulitokea majira ya mchana na kwamba wakiwa shambani waliona moshi ukitokea katika moja ya chumba cha nyumba hiyo.

"Tulikuwa shambani, ghafla tukasikia harufu ya kuteketea vitu vya plastiki. Baada ya dakika tano, tukaanza kuona moshi ukivuka upande wa kushoto, ndipo tulipolazimika kufuatilia na kubaini wapi ulikotokea,"alibainisha William.

Ambos Chuwa, shuhuda mwingine, alisema walipiga kelele na watu waliokuwapo karibu walifika na kujaribu kuwaokoa watoto hao bila mafanikio.

"Inaonekana watoto hao walikuwa ndani wenyewe na wazazi walikuwa kwenye mihangaiko ya utafutaji. Wote ni wajukuu wa mzee Kimaro kwa mtoto wake wa kike na wa kiume. Haijulikani walifanya nini humo ndani, nyumba imeteketea yote," alisema Fabian Moris.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Raphael Mushi, alisema walipofika katika eneo hilo hapakuwa na mtu mzima na jitihada zilianza za uzimaji wa moto kwa ushirikiano na wananchi bila mafanikio.

"Watoto wawili wameteketea moto. Nyumba imeisha ingawa tunashukuru wananchi wamejitokeza kuzima pamoja na jeshi la uokoaji walifika kwa ajili ya uokozi ingawa hakuna kilichookolewa,"alisema Mushi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, alisema tukio hilo lilitokea juzi watoto hao wakiwa wamelala wakati baba yao alipokwenda dukani kununua sigara.

"Baba wa hawa watoto aliondoka muda mfupi kwenda kununua sigara dukani wakati anarudi akakutana na moshi mkubwa ukitoka ndani ya nyumba hiyo. Watoto wote wawili walioteketea kwa moto," alisema Kamanda Maigwa.

**KABWELA** — **Na Fadhili Mohammed**





Ofisa Msimamizi wa Kodi Mwandamizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Joyce Ng'oja (kushoto), akikagua risiti ya EFD katika eneo la Mbagala Rangi Tatu, Dar es Salaam jana, wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WB yaipiga jeki Tanzania tril. 1.2/- maji vijijini, afya ya mama na mtoto

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya Dunia (WB) imeipatia Tanzania Dola za Marekani milioni 550 (Sh. trilioni 1.264) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mpango endelevu wa huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini pamoja na uboreshaji wa afya ya mama na mtoto.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam juzi wakati wa utiaji saini wa mikataba hiyo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema fedha hizo ni mkopo wa masharti nafuu.

DK. Mwigulu alisema mradi wa usafi wa mazingira vijijini umetengewa Dola za Marekani milioni 300 (Sh. bilioni 689.51) wakati mradi wa afya ya mama na mtoto umepokea Dola za Marekani milioni 250 (Sh.bilioni 574.59). Alisema malengo ya miradi ambayo mikataba yake imesainiwa inaendana na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano (2021/22- 2025/26) pamoja na Dira ya Zanzibar ya mwaka 2050.

Waziri alisema pia ni sehemu ya ajenda kuu ya serikali inayolenga kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu, wenye lengo la kufikia vipaumbele vya mpango. Alivitaja vipaumbele hivyo ni kuongeza upatikanaji wa vyanzo vya maji salama hususani katika maeneo yenye upungufu na matatizo ya upatikanaji wa maji vijijini na uboreshaji wa usafi wa mazingira pamoja na utoaji wa huduma bora za afya za uhakika Tanzania Bara na Zanzibar. Mkataba wa fedha za ziada kwa ajili ya mpango endelevu wa maji na usafi wa mazingira vijijini, alisema unakwenda kukamilisha juhudi katika kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini na kuimarisha uwezo wa taasisi za sekta kuendeleza utoaji wa huduma bora.

"Mradi wa afya ya mama na mtoto utaongeza wigo wa utoaji na kuboresha huduma muhimu za afya kwa kuzingatia afya ya mama na mtoto Tanzania Bara na Zanzibar," alisema Dk. Mwigulu.

Alisema kusainiwa kwa mikataba hiyo kumeiwezesha WB kuongeza kiwango cha fedha walizozitoa kama mkopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo hapa nchini kufikia Dola za Marekani bilioni 7.8 tangu ushirikiano ulipoanza. Mkurugenzi Mkazi wa WB Tanzania, Nathan Belete, alisema Tanzania imefanya maendeleo makubwa katika kuimarisha huduma za afya kwamba kwa mwaka 2000 hadi 2019 wastani wa umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 51 hadi 65.

Alisema hata vifo kwa watoto chini ya umro wa miaka mitano vimepungua kwa robo tatu. Kwamba uwapo wa chanjo nako umesaidia kupunguza maambukizi ya ugonjwa mbalimbali kama vile kuharisha, malaria na UKIMWI.

## Sita wajitokeza kumrithi Mrema TLP

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Tanzania Labour (TLP), kimefunga dirisha la utoaji fomu za kuomba kuwania nafasi mwenyekiti wa taifa wa chama hicho, huku wanachama sita wakiwa wamejitokeza kuwania nafasi hiyo.

Akizungumza na Nipashe Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa TLP, Richard Lyimo, alisema dirisha la utoaji fomu lilifungwa jana saa 4:00 asubuhi na kuwataja wanachama hao kuwa ni Dominata Rwechungura na Ivan Maganga.

"Wanachama wengine ni Abdul Shangawe, Stanley Ndamugoba, Kinanzaro Mwanga na mimi Richard Lyimo, ambao sasa tutachuana katika mkutano mkuu wa uchaguzi utakaofanyika Machi 6, mwaka huu," alisema Lyimo.

Alisema awali walipanga kufanya uchaguzi huo jana lakini wakaahirisha ili kuwapa muda wanachama wajitokeze zaidi na kwamba hatua hiyo imesaidia kuongezeka wanaowania kutoka watatu wa awali hadi sita.

"Ninaamini kila mmoja anayetaka kugombea amepata muda wa kutosha wa kutafakari na kuchukua fomu au kufanya uamuzi mwingine wenye lengo la kuendelea kuimarisha demokrasia ndani ya chama chetu," alisema.

Alifafanua kuwa Machi 5, mwaka huu, Halmashauri Kuu ya TLP itakutana ili kuweka mambo sawa kabla ya uchaguzi huo wa kumpata mwenyekiti wa taifa, wajumbe wawili wa baraza la wadhamini na katibu mipango wa chama.

Lyimo alisema uchaguzi wa mwenyekiti wa chama hicho utahudhuriwa na wajumbe 142 wa mkutano mkuu bila kushuhudiwa na wawakilishi kutoka katika vyama vingine vya siasa.

Pia alisema chama hicho kimepitia hatua nyingi na kwamba sasa wameamua kujipanga upya, ili kuhakikisha kinashiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Nafasi ya Mwenyekiti wa TLP kwa sasa inakaimiwa na Hamad Mkadam aliyechaguliwa na sekretarieti ya chama hicho Septemba, mwaka jana, wiki chache tangu aliyekuwa Mwenyekiti, Augustine Mrema kufariki dunia.

# Chongolo aishukia TIC kuhusu wawekezaji

**Na Augusta Njoji,** IKUNGI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amekishukia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa kuishia kuwasajili wawekezaji kwenye makablasha badala ya kuwatembelea kujua kero zao na kuzitatua ili uwekezaji uwe na tija kwa taifa.

Akizungumza juzi kwenye ziara yake akiwa na sekretarieti ya chama hicho wilayani hapo alipokuwa akikagua mradi wa kilimo cha alizeti unaotekelezwa na Kampuni ya Alfardaws, Chongolo alisema kituo hicho kina jukumu la kutoa kibali kwa wawekezaji na kuhakikisha mahitaji muhimu yanawafikia kwenye maeneo yao lakini hakifanyi hivyo.

"Bado tumeshindwa kutoka kuwa watu wenye kutimiza wajibu kuwa watu wenye kutafuta matokeo. Lazima kama nchi hili tulifanye kwa dhati ya mioyo yetu. Hatuwezi kuwa na namba ya wawekezaji tuliowasajili hatujui huko wanafanya nini, wanawezeshwaje kufikia uwekezaji uliokusudiwa," alisema.

Katibu mkuu huyo alisema mwekezaji Alfardaws kwa zaidi ya miezi minne ana tatizo la kutounganishiwa umeme ambao uko umbali wa kilometa tatu.

"Lengo hapa ni kutoa ajira 70 hiki ni kigezo cha haraka cha kuhakikisha anapata umeme ambao hata gharama zake hazizidi Sh. milioni 100. Mradi huu ni uwekezaji mkubwa hebu tufanye jambo tuhakikishe ndani ya mwezi mmoja umeme utakuwa umefika," alisema. Chongolo alisema TIC wanapoitwa hutoa idadi kubwa ya wawekezaji lakini ni muhimu kuwatembelea kwenye maeneo yao ili kuona tija ya uwekezaji wao. Aidha, alishauri Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kutenga maeneo ya uwekezaji ambayo yatasaidia kuchochea uchumi wa eneo hilo.

"Kuna ombi la nyongeza ya ardhi ya mwekezaji, niwaombe mwangalie namna ya kumwongezea ardhi, lakini nini mpango wenu wa kuhakikisha hata zinapatikana hekari 40,000 zinaandaliwa vizuri kwa ajili ya wawekezaji wa namna hii," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema mwekezaji huyo kutoka Jordan ametokana na matunda ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kufungua milango ya uwekezaji.

Awali, mwekezaji Anass Kaseeh aliomba kusaidiwa kupatiwa huduma hiyo kwa kuwa tangu wamefanya maombi hawajafanikiwa kupata.

"Tumeshaleta mashine zote na tumeshachimba visima vitatu vya maji kati ya 24 vinavyohitajika na mfumo wetu wa umwagiliaji kwenye mradi unahitaji umeme mkubwa hadi sasa hatuna umeme tulishaomba, tunaomba serikali itusaidie na sisi tuko tayari kushirikiana kurahisisha mchakato," alisema.

Akisoma taarifa ya mradi huo, mhandisi wa kampuni hiyo, Edwin Nambiza, aliomba serikali isaidie kuharakisha mchakato kubadili usajili na umiliki wa ardhi hiyo ili kampuni imiliki kupitia TIC. Aidha, alisema kampuni inahitaji ardhi ya mita za mraba 6,000 na ardhi iliyopo ni mita za mraba 1,700 huku akisema ipo tayari kulipa gharama kama ardhi hiyo itapatikana. Pia alisema wanakabiliwa na ukosefu wa wafanyakazi kutokana na wanaozunguka eneo la mradi kutokuwa na ari ya kufanya kazi hali inayolazimu kampuni kutafuta kutoka nje ya wilaya na mkoa. "Vijana walipo hawana ari kwa kuwa wakilipwa malipo ya siku moja hawaji kazini siku tano, hii changamoto kubwa inasababisha kampuni kuingia gharama,"alisema.

Katika hatua nyingine, Chongolo akiwa mgodi wa dhahabu wa Shanta, alisema kumekuwa na tatizo la umeme kwa wawekezaji na kuitaka Tanesco kuweka msukumo wa kujenga vituo vya kupoozea umeme kwenye maeneo yenye uwekezaji mkubwa ikiwamo ukanda wa Singida.

Kauli hiyo imekuja baada ya Mhandisi Ernest Mrema wa mgodi huo, aliomba kuwezeshwa kupitia Tanesco kupatikana umeme wa kutosha wa uhakika wa kuendesha mitambo ya mgodi ili kupunguza matumizi ya mafuta kuzalishia umeme.



## Wakulima wapata neema ya matrekta

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KAMPUNI ya Equity for Tanzania Limited (EFTA), imeanza kutoa mikopo ya matrekta kwa wakulima bila dhamana ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kukuza sekta ya kilimo nchini.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati akifungua mafunzo kwa wakulima juu ya matumizi sahihi ya matrekta, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya EFTA, Nicomed Bohay, alisema lengo la kuanzisha mpango huo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kukuza sekta ya kilimo.

Kwa mujibu wa Bohay licha ya kuwakopesha matrekta hizo pia watatoa mafunzo kwa wakulima hao, juu ya matumizi sahihi ya trekta, utunzaji wa fedha pamoja na kulima kilimo chenye tija.

"Mafunzo haya yataanzia kwa wakulima zaidi ya 200 katika eneo la Kateshi mkoani Manyara kisha Kibaigwa (Dodoma), Kahama (Shinyanga) na Kilombero (Morogoro) lengo ni kuhakikisha wakulima wanayatumia matrekta hayo kwa tija.

Mkurugenzi wa CMC, Sokib Eltaff, alisema uwapo wa mashine hizo itasaidia kuongeza matumizi ya mashine katika sekta ya kilimo na kuongeza uzalishaji tofauti na kutumia jembe la mkono.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima waliopata mkopo huo, Emmanuel Mwangi alisema anaishukuru EFTA kwa sababu imebadilisha maisha yake baada ya kupata mkopo wa trekta kwa mara ya kwanza mwaka 2016.

"Leo nimekopeshwa trekta ya tatu, ya kwanza nilikopa mwaka 2016, ya pili mwaka 2021 na zote nimerejesha bila usumbufu kwa sababu ziliniwezesha kuongeza kipato changu na kubadilisha maisha ya familia yangu, "alisema.

Aidha, alisema wakati anakopa trekta mwaka 2016 alikuwa na shamba hekari 10 eneo la Magugu lakini kwa sasa anamiliki hekari 80 na zimetokana na trekta alizokopeshwa na kulipa kwa muda wa miaka mitatu na alilipa baada ya kuvuna.

# Wakazi Mianzini wanaopitiwa na ujenzi wa barabara kulipwa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI imeahidi kulipa fidia kwa wananchi wa Mianzini wanaopitiwa na ujenzi wa Barabara ya Olemringaringa - Ngaramtoni Juu (Km 8.5) inayoendelea kujengwa kwa kiwango cha lami.

Hayo yamesemwa juzi jijini Arusha na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, wakati alipokagua hatua za utekelezaji wa mradi huo wenye urefu wa kilometa 18 unaoanzia Mianzini - Olemringa - Ngaramtoni Juu na Olemringaringa - Sambasha - Timbolo ambao umefikia asilimia 23 ya utekelezaji wake.

"Sehemu ambazo barabara imefuata wananchi tutawalipa baada ya kazi ya kutathmini kumalizika kwani ni haki yao," alisema Prof. Mbarawa.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo ni ahadi iliyotolewa na Hayati Rais John Pombe Magufuli kujengwa kwa kiwango cha lami na unafadhiliwa na Tanzania kwa asilimia mia na utatekelezwa kwa muda wa miezi 15.

Profesa Mbarawa alisema ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Agosti, 2023.

Prof. Mbarawa alitoa wito kwa Meneja wa Mkoa wa TANROADS kusimamia ujenzi wa barabara hiyo na kuhakikisha thamani ya fedha na ubora wa barabara unaonekana pale ujenzi utakapokamilika.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Steven Zelothe, alimpongeza Rais Samia kwa kuwa wananchi wanaendelea kuona juhudi za dhati zinazoendelea kufanywa na serikali hasa kwa Mkoa wa Arusha.

Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, alisema kuwa mradi huo utakapokamilika utarahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa haraka wa wakazi wa maeneo hayo na kuongeza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Arusha, Mhandisi Reginald Massawe, alisema barabara hiyo imesanifiwa kubeba ekseli za magari zipatazo milioni tatu zenye uzito wa tani nane kila moja katika muda wa miaka 20.

Amesema kuwa hadi sasa mkandarasi ameshaleta mitambo, vifaa na magari yanayotumika kwenye kazi za ujenzi wa barabara hiyo na matumaini yao mradi utakamilika kama ulivyopangwa.



Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo (kushoto), akikabidhi kadi za pikipiki mbili aina ya TVS kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa mjini Moshi jana, kwa ajili ya kulisaidia jeshi hilo kukabiliana na uhalifu. **PICHA: MARY MOSHA**

# Wahukumiwa jela madai kukutwa nyara za serikali

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, imewahukumu watu wanne kila mmoja kutumikia kifungo cha miaka 22 gerezani baada ya kukutwa na nyara za serikali bila kuwa na kibali.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Victor Kimario.

Kimario aliwataja waliohukumiwa kwenda ni Langay Surumbu (55) mkazi wa Kijiji cha Endadish wilayani Babati, Mussa Kwanangw (42), Atylu Khamis (36) na Haayuma Lohay(36) wote wakazi wa Kijiji cha Endadish.

Hakimu huyo alisema washtakiwa hao amewatia hatiani pasipo shaka baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili. Aidha, alisema upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi sita na utetezi walikuwa wanajitetea wenyewe isipokuwa mshtakiwa mmoja aldai kwamba atakuwa na shahidi mmoja.

Alisema washtakiwa hao amewatia hatiani kutumikia kifungo cha miaka 22 kila mtu kutokana na kukiuka kifungu cha 86(1)(2)(c)(iii) cha Sheria ya Wanyamapori Sura ya 283 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022. Hakimu alisema washtakiwa walikamatwa Novemba 22, mwaka jana katika Kijiji cha Endadish wakichinja mnyamapori aina ya tandara mkubwa.

Hata hivyo, washtakiwa walikamatwa na kilogramu 157.6 za nyama zenye thamani ya Dola za Marekani 2,200 sawa na Sh. milioni 5.053 fedha za kitanzania.

Mawakili wa serikali wakiongozwa na Rusticus Mahundi na Abood Komanya, walidai hawana kumbukumbu za nyuma za uhalifu kwa washtakiwa hao ila waliomba mahakama iwape adhabu kali kwa kuwa wanyamapori ndiyo sekta inayochangia pato kubwa la taifa.


Mahundi alidai kuwa washtakiwa kutenda uhalifu huo ni kudidimiza harakati za kuongeza mapato ya taifa hivyo wamefanya kosa hilo kwa makusudi ili pato la taifa lisikue.

Washtakiwa hao walipopewa nafasi ya kujitetea mshtakiwa namba moja alidai anaomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ni mgonjwa.

Mshtakiwa wa pili aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa anaishi na mama yake na ni mzee, macho yake hayaoni na kaka yake amepooza na anasomesha watoto wanne.

Mshtakiwa wa tatu aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ana watoto wanne na watatu wanasoma shule na anawalea mwenyewe. Mshtakiwa wa nne aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa anaishi na mama yake ambaye ni mlemavu na yeye ndio anamtegemea.

Baada ya utetezi huo Hakimu alisema amezingatia utetezi wao na walistahili kuonewa huruma lakini sheria imetaja kiwango cha adhabu kisipungue kifungo cha miaka 20 jela kulingana na kosa walilofanya.





## Wanaoishi visiwani waiomba serikali kuwajengea shule

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKAZI wa Mkoa wa Mwanza wanaoishi maeneo ya visiwani wameiomba serikali kujengewa shule katika maeneo ya visiwa ambavyo havina huduma hiyo ili kuwanusuru idadi kubwa ya wanafunzi wanaokatisha masomo.

Wamesema idadi kubwa ya wanafunzi wanakatisha masomo kwa kushindwa kusafiri kwa kutumia mitumbwi.

Wakizunguza na Nipashe baada ya mkutano wa pamoja wa wadau wa kupinga vitendo vya ukatili, majadiliano yaliyokutanisha mashirika yasiyo ya kiserikali chini ya bodi ya uratibu wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali walisema miongoni mwa kero zinasababisha ongezeko la watoto wa mitaani ni kukosekana kwa baadhi ya huduma za elimu pamoja na mindombinu ya usafiri visiwani

Mmoja wa wakazi hao Juvenary Matagiri alisema: "Hali ya usafiri kwa wanafunzi wa visiwani kufuata shule bado siyo rafiki kutokana na baadhi ya visiwa kukosa shule na kuwafanya wanafunzi hao kufuata shule katika visiwa jirani na kusabisha baadhi yao kufanya shughuli nyingine za kibiashara".

Mwenyekiti wa bodi ya uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali, Mwantumu Mahiza aliyataka mashirika hayo kuacha kuwatumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu kujinufaisha badala yake waunganishe nguvu ili kuwasaidia. Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala aliyataka mashirika hayo kushirikiana na serikali katika kupambana na kero hizo zinazosababisha ukatili kwa watoto hao na kuwakosesha haki zao za msingi.

# Imani potofu yakwamisha utolewaji chanjo corona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UTOLEWAJI wa kinga dhidi ya ugonjwa wa virusi vya corona umeendelea kusuasua mkoani Shinyanga, kutokana na uwapo wa imani potofu dhidi ya chanjo hiyo.

Hali hiyo imesababisha wazee kuwa hatarini kupata maambukizi kutokana na kukosa huduma hiyo.

Katibu wa Baraza la Wazee mkoani Shinyanga, Anderson Lyimo, aliyasema hayo wakati wa kikao kazi na mabalozi wa nyumba kumi kilichohusu uhamasishaji wa chanjo ya corona kwa makundi ya wazee, vijana na wanawake wa Kata ya Tinde na Didia wilayani Shinyanga chini ya Shirika la WEADO.

Alisema bado kuna uhitaji wa elimu dhidi ya chanjo hiyo ili kusaidia wananchi kujikinga dhidi ya ugonjwa huo.

Lyimo alisema wazee wengi wamekuwa hawajitokezi kupata huduma hiyo kwa kisingizio kuwa wakipata chanjo watapunguza siku za kuishi pamoja na viungo vya mwili kudhoofika.

"Mimi nimepata chanjo ya corona tangu Agosti mwaka 2021 na sijapata madhara yoyote hadi sasa na afya yangu ni imara, na baadhi ya magonjwa madogo ambayo yalikuwa yakinisumbua mfano mafua na vikohozi hayapo tena, hivyo nawasihi wazee wenzangu hasa wa vijijini jitokezeni mpate chanjo ni salama na haina madhara yoyote puuzeni imani potofu,"alisema Lyimo.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Kata ya Didia wilayani Shinyanga, Engelbert Kidutu, alisema hakuwa tayari kupata chanjo hiyo lakini baada ya mke wake kuona afya yake inateteleka mwaka jana akampeleka kupata chanjo na hakupata madhara yoyote.

Ofisa Miradi kutoka Shirika hilo la WEADO, Winnie Hinaya, alisema wanaendesha mradi huo wa uhamasishaji chanjo ya corona kwa wazee, vijana, wanawake pamoja na kupinga vitendo vya ukatili na uinuaji uchumi katika kata sita za wilayani Shinyanga ambazo ni Tinde, Didia, Masengwa, Usanda, Iselamagazi na Solwa kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia watoto Duniani (UNICEF).



Katibu wa Baraza la Wazee Kata ya Didia, wilayani Shinyanga, Engelbert Kidutu (kulia), akipatiwa chanjo ya UVIKO-19 na Ofisa Afya wa Kata, Edwardina Maganga, baada ya kuhamasishwa na kuondolewa imani potofu kuhusu usalama wa chanjo hiyo, wakati wa kampeni ya Shirika la Women Elderly Advocacy and Development Organization (WEADO), lilipokutana na mabalozi wa kuhamasisha chanjo katika kata za Tinde na Didia, wilayani humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wanafunzi wasoma chini kisa ukosefu wa darasa

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WANAFUNZI wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Ilamba iliyopo Kata ya Igwamanoni Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga wanalazimika kusomea chini ya miti baada ya halmashauri kutokamilisha darasa lililojengwa na wananchi ambalo linatakiwa kutumiwa na wanafunzi hao.

Shule hiyo ina wanafunzi 780, wanafunzi wa kike 399, wa kiume 381, kati ya hao wanafunzi 69 wa awali wanalazimika kusomea chini ya miti.

Hivyo, wameiomba serikali kuingilia kati kutatua kero hiyo ili kuwanusuru katika kipindi hiki cha mvua za masika ambapo wanalazimika kusoma kwa awamu.

Akizungumza na Nipashe Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Marry Lema, alisema boma la darasa lilijengwa kwa nguvu za wananchi na liko hatua za mwisho ya ukamilishaji.

Alisema: "Vifaa vya ukamilishaji wa darasa hilo vipo ikiwamo misumari kilo 25, mbao zipo za aina zote pamoja na mabati 64 ya kuezekea, lakini tunashangaa kuona viongozi wa kata wanashindwa kuingilia kati ya kulikamilisha.

Kama wameweza kusogeza huduma ya maji safi na salama shuleni wanashindwa vipi kukamilisha darasa hilo."

Alisema shule inaupungufu wa walimu sita hasa wa masomo ya hesabati na sayansi kwani walipo ni 11 na hawatoshelezi mahitaji ya shuleni.

Kadhalika alisema baadhi ya wanafunzi wanalazimika kufundisha masomo hayo lengo likiwa ni kuhakikisha wanafunzi hawakosi masomo yao na kushindwa kufanya vema kwenye mitihani yao ya mwisho.

Mkazi wa Kata ya Igamwamanoni, Isabela William, alisema kitendo cha kushindwa kukamilisha darasa hilo kwa wakati kinawakatisha taama ya kuendelea kujitoa katika kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo mashuleni.

Akijibu Malalamiko hayo, Ofisa Elimu wa Shule za Msingi wa Halmashauri hiyo, Mwalimu Charles Mburu alisema walitoa Sh.milioni 12.5 kwa ajili ya ukamilishaji wa darasa na sasa kinatumika na kuhoji kama kunachumba kingine kimejengwa kwa nguvu za wananchi na vifaa vya ukamilishaji vipo kwanini wasikamilishe.

Mburu alisema walipeleka Sh. milioni 46.5 katika shule hiyo kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 40, kwamba matundu 38 yamekamilika na kuwekewa mifumo yote ya maji na kuwataka kuvitunza na kuwanufaisha wanafunzi wote.

ama
ALHAMISI MACHI 2, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



## Surua kuua watoto, yamkurupusha waziri kuibukia Katavi na kampeni

Ukurasa 12



## Mradi DMDP: Miaka 10 imeizawadia Dar barabara, taa mitaani, mifereji...

Ukurasa 13

# Ujue 'umama' wake mkuu wa nchi kwenye sera afya, nafasi ya mzazi

• Awafuata waliko; awasifu, elekeza, 'awapasha' majeuri

**Na Mwandishi Wetu**

KISERA, Tanzania ilipokuwa taifa changa haina miaka mingi baada ya uhuru, vita endelevu iliyoko hadi sasa kusaka maendeleo ya nchi, ilizama katika kutafutia watu maisha bora katika sura inayokidhi ya zama hizo.

Muasisi wa taifa, Rais Julius Nyerere, katika angalizo lake la awali alikumbatia mambo makuu matatu vitani; ujinga, umasikini na maradhi.

Ndio imekuwa ajenda ya taifa hadi sasa, ikiwa ni mashiko katika mipango ya maendeleo ya nchi na kimataifa, mathalan kupitia mashirika ya Umoja wa Mataifa; WHO la afya na UNICEF la watoto.

Kwa mujibu wa harakati za awali za taifa Tanganyika, Mpango wa Maendeleo wa Muda Mfupi, 1961 hadi 1964, pia Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano ya Tanzania; 1964 hadi 1969, hayo matatu hayajasahaulika katika awamu sita za uongozi nchini tangu uhuru.

### AJENDA AFYA

Kurejea ajenda ujinga na maradhi, kwa kiasi kikubwa vinategemeana na ukamilifu wake una tafsiri kubwa katika kufuta umasikini. Hiyo inatokana na uhalisia kwamba, panapo ujinga na maradhi, inaipa gharama kubwa serikali na mtu mmoja mmoja, huku uwezo wa kuzalisha na hali ya utegemezi inakomaa.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwapongeza na kuwapa zawadi wanawake waliojifungua katika jengo jipya la Huduma ya Afya ya Mama na Mtoto, kwenye Hospitali ya CCBRT, Dar es Salaam, mnamo Julai 05 mwaka jana. **PICHA: MTANDAO.**

Ni sehemu ya yaliyoko kwenye kanuni na nadharia za uchumi inayosisitiza kwamba, vyanzo vikuu vya uzalishaji katika uchumi zinajumuisha; nguvukazi, mtaji, ardhi na taasisi au ujasiriamali unaoendesha uzalishaji huo.

Hata hivyo, katika nadharia za sasa za uchumi zinaipa kipaumbele nguvukazi au mtu, kwani ndio inaandaa mipango vilevile namna ya kusimanmia vyanzo vingine tajwa vya uzalishaji.

Hauikushangaza zama iliyopo, eneo hilo linaboreshwa zaidi na ushuhuda wake ukianzia penye taaluma kama Usimamizi wa Wafanyakazi (Personnel Management), katika miongo miwili iliyopita, ikiboreshwa kimataifa kuwa na sifa ya ziada ya ubunifu, kwa sasa ikiitwa Rasilimaliwatu (Human Resource Management).

Kwa lugha rahisi, watu na nguvu kazi yao wametambuliwa kuwa hazina kubwa kwa maendeleo kitaifa inayofuta umasikini. Hapo inamaanisha, usalama wake chini ya ulinzi afya ni muhimu maradufu.

### NAFASI ALIKOSIMAMIA

Vivyo hivyo, kama walivyo watangulizi wake watano katika uongozi kitaifa, kwenye ajenda hizo tatu za kihistoria nchini, kipengele cha afya, Rais Dk. Samia amezama katika miradi minne mikuu, inayojumuisha Mpango wa Maendelo ya Afya ya Msingi (MMAM) ulioanza mwaka 2008.

Mengine ni kuhitimisha changamoto kubwa za kiafya kama vile milipuko ya magonjwa na maboresho ya viwango vya tiba na huduma za kisasa hospitali kuu, kama vile Muhimbili (MNH) na Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) Dar es Salaam, pia Benjamin Mkapa ya Dodoma.

Kuna maeneo makuu mawili Dk. Samia anakovaa uhusika wake wa 'umama', akijikita na kuzama kwenye utashi wa nafsi yake, kinamama na watoto; akipigana kuwatunza watoto, mama na mahitaji yao.

Akashuhudiwa, mwaka juzi, Rais kajipenyeza katika jumuiya ya wanamichezo, akiwaahidi kuchangia shilingi milioni 15 kwa taasisi inayojishughulisha na kuwasemea wenye magonjwa adimu yasiyo na tiba, yakitajwa duniani yako zaidi ya 7,000.

Ni taasisi ya mtoto Ali Kimara (10) mkazi wa Kimara Dar es Salaam, alikoahidi kutoa fedha hizo kuchangia changamoto ya upumuaji kwa takribani miaka nane sasa, ahadi iliyoendana na kupata 'sapoti' kutoka taasisi GSM, iliyotoa shilingi milioni 10.

Ulikuwa mjumuiko wa burudani, mechi ya kirafiki, Dar es Salaam, baina ya timu ya soka Yanga na kutoka Somalia. Mtoto Ali amekuwa akitumia mashine ya umeme kumsaidia kupumua saa zote, pia mtungi wa gesi, umeme unapokatika.

Mzazi wa Ali aitwaye, Sharifa Mbarak, akasisitiza kuwa tayari walishaanza kuzungumza na Hospitali ya Taifa Muhimbili na Idara ya Utafiti, katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Tiba (MUHAS) kwa ajili ya kuanzisha tafiti za magonjwa hayo adimu nchini Tanzania.

Mnamo Desemba mwaka 2021, Rais Dk. Samia akitimiza miezi nane kazini, vilevile Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) katika hafla ya kutimu miaka 75, baadhi ya watoto wakamwandikia barua Rais Dk, Samia Suluhu Hassan, kujadili changamoto zinazowakabili.

Ni mkusanyiko ulioonyesha 'umama' wa Rais Dk. Samia, aliyesomewa waraka mtoto akisaidiwa na mwanaharakati wa masuala ya vijana, Meena Ally na mshairi

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Surua kuua watoto, yamkurupusha waziri kuibukia Katavi na kampeni



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, katika kampeni ya kukabili mlipuko wa surua mkoani Katavi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

**Na Yasmine Protace**

SASA katika baadhi ya maeneo nchini kumetangazwa mlipuko wa maradhi surua, ambayo yaliwahi kuzuka zama zilizopita na hasa kwa watoto, ikiwa na kasi kubwa ya uambukizaji.

Pia, kuna wakati ikapewa jina Rubeola, ikibeba sifa katika homa na ugumu wa kupumua. Kitaalamu, inatajwa kuwa ya hatari na yenye historia ya kuua, hususan Afrika na Kusini- Mashariki mwa Asia, waathirika wakuu ni watoto. Vilevile, inatajwa kuzuilika kirahisi, ikianzia na chanjo.

Surua inaenezwa zaidi na virusi aina ya 'morbillivurus paramyxvirus' vinavyoenea haraka kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, ikipitia kwenye hewa na hasa mgonjwa anapokohoa au kupiga chafya.

Ni ugonjwa unaoathiri watu wa rika zote, licha ya kuwa zaidi ni watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Sasa kuna mlipuko unaotangazwa katika mikoa mbalimbali, ikiwamo Katavi.

**WAZIRI UMMY**

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema serikali sasa imewaelekeza wazazi na walezi mkoani Katavi, kuwapeleka watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano wakapate chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa surua.

Agizo hilo alilitoa akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua hali ya utoaji wa huduma za afya na kuzindua kampeni ya kuongeza kasi na hamasa ya chanjo ya surua kwa Halmashauri ya Mpimbwe. wilayani Mlele, mkoani Katavi.

Ummy anasema, anayo mamlaka ya kisheria kupitia Sheria ya Afya ya Jamii kuamua chanjo za watoto za kuwakinga na surua si ya lazima, hivyo anawataka wakuu wa wilaya na mikoa kuwachukulia hatua wazazi na walezi watakaoshindwa kuhakikisha watoto wao wanapata chanjo ya surua.

"Wakuu wa wilaya na wakuu wa mikoa, mhakikishe watoto wanapata chanjo,kama kuna mzazi au mlezi atashindwa kumpeleka mtoto kupata chanjo achukuliwe hatua," anasema.

Anaeleza msimamo wake kwamba, hatokubali kwa nafasi yake ya serikali, kuona watoto wanapoteza maisha, ilhali wana uwezo wa kuwakinga kwa kuwapatia chanjo ya surua mapema.

Waziri anawaelekeza wazazi na walezi mkoani Katavi kupeleka watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano kupata chanjo ya kujikinga na surua, alipokuwa anazindua kampeni ya kuongeza kasi na hamasa ya chanjo ya surua katika Halmashauri ya Mpimbwe, wilayani Mlele.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, kuna watoto zaidi ya 400,000 waliokosa chanjo hiyo, huku tayari kuna vifo vilivyoripotiwa hadi sasa 13, kati yake 11 vimetokea majumbani na viwili hospitalini, sababu kuu ni wagonjwa kucheleweshwa kufika katika vituo vya huduma za afya.

"Leo tupo hapa Majimoto Mpimbwe kuwaunga mkono wana Mpimbwe na wana Majimoto, ili tuishinde surua. Lazima, watoto wote umri chini ya miaka mitano wakamilishe dozi ya chanjo ya surua", anaagiza.

Pia, anafafanua takwimu ilivyo, katika kila watoto 100 wanaougua surua katika Halmashauri ya Wilaya Mpimbwe, 40 wanatoka katika Kata ya Majimoto.

Hata hivyo, Waziri Ummy anasema hadi sasa kazi ya chanjo inaenda vizuri na kupitia ziara hiyo, amezindua msafara wa kampeni ya bodaboda na magari 10 yanayotoa elimu na hamasa ya chanjo kwa wananchi Mpimbwe, ili kusambaza uelewa wa kupeleka watoto kupata chanjo ya surua mapema.

Pia, anasema kuna magari mengine matano yatakayopelekwa katika Halmashauri ya Wilaya Mlele na matano Halmashauri ya Wilaya Tanganyika, kufanya kazi hiyo wakipita 'nyumba kwa nyumba' kuhakikisha kila mtoto wa umri chini ya miaka mitano akapatiwe chanjo, akihimza umakini na ujasiri wao kulifanikisha hilo.

Waziri Ummy anaelimisha kwamba, kwa aliyepata chanjo, hata akipata surua, haitakuwa kali tofauti na asiyechanjwa, akitoa mfano wa hatua kama hiyo imewanusuru wengi na maradhi Uviko-19.

Pia, anawataka waganga wa tiba asilia, nao washiriki kuhimiza wateja wao chanjo ya surua, kwa kuwaelekeza kwenda kwenye vituo vya afya wakahudumiwe.

# Ujue 'umama' wake mkuu wa nchi kwenye sera afya, nafasi ya mzazi

**INATOKA UK. 11**

maarufu, Mrisho Mpoto.

Miezi nane baadaye, Rais Dk. Samia katika hafla nyingine ya kufungua jengo la huduma ya afya ya mama na mtoto katika hospitali ya CCBRT, Dar es Salaam, akakumbusha lengo la ujenzi huo ni kumpatia mwanamke huduma bora ya uzazi tangu ujauzito, kujifungua na penye uangalizi wa mzazi na mwanawe mchanga.

Ni jengo linalowezesha kuhudumia wanawake 300 kwa siku, likiwa na vitanda 140 na vyumba vinane vya kujifungua, suala lililotajwa katika haflla hiyo ni ulingo wa kupatikana huduma za uchunguzi mapema na matibabu ya watoto waliozaliwa na ulemavu.

Rais Dk. Samia anafafanua nafasi ya serikali kwamba ni utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo kati ya mwaka wa fedha 2021/2022 hadi mwaka wa fedha, 2025/2026, pakilengwa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, kutoka 321 kwa kila vizazi 100,000 hadi 220.

Pia, akaielekeza Wizara ya Afya kuhakikisha madaktari bingwa wanapatikana katika hospitali za wilaya, ili kuwezesha huduma zao muhimu.

"Vifo vya watoto wachanga wenye umri chini ya siku 28 vimepungua hadi kufikia vifo saba kwa kila vizazi hai 1000," anatamka rais ni hatua anayochukua kukabiliana na magumu ya huduma.

Mathalan, wakati fulani gazeti hili likaripoti habari za wilayani Uvinza, Kigoma, vijiji vya Katumbi na Nkonkwa, kata ya Buhingu, kuwapo zahanati mbili ambazo kila moja zilikuwa na mtumishi mmoja.

Pia, anawaelekeza wataalamu tiba na wauguzi wote nchini, anachokitaja kuacha dharau kwa wajawazito na kuwaepushia vifo vinavyoweza kuzuilika.

Rais anasema katika mikakati ya kuboresha huduma kwa wajawazito na watoto wachanga, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma vya madaktari bingwa wa magonjwa ya kinamama na uzazi, wameanzisha mfumo wa kupitia takwimu za vifo vya kinamama na watoto wakati wa kujifungua.

Anaeleza hadi sasa, takwimu zinaonyesha asilimia kubwa ya wanaofariki ni kutokana na mapungufu ya watoa huduma, akirejea mfano wa tukio la wauguzi kumuamuru mlinzi asiwafungulie mlango wagonjwa wahitaji.

Hapo anatumia hoja kielelezi ya tukio akinena: "(Mkunga) anaambiwa kuna kinamama wanataka kujifungua, anajibu 'nesi amesema nisifungue mlango.' Mpaka kinamama wamejifungulia getini, wengine wamekimbizwa walikokimbizwa.

"Dharau hizi, uzembe huu, kutokuwa na usimamizi wa kutosha kunaleta maafa kwa wanawake wakati wa kujifungua. Nadhani hatupaswi kupata hukumu hii, ingawa mwisho yakitokea tunasema 'Mungu ndivyo alivyoandika'...."

"Niombe sana Waziri (wa Afya) na watu wako mjitahidi kusimamia hayo mambo kule kwenye vituo vya kutolea huduma."

MAZINGIRA

# Mradi DMDP: Miaka 10 imeizawadia Dar barabara, taa mitaani, mifereji...

**Na Beatrice Shayo**

MIAKA ya nyuma kabla 2016, miundombinu ya mkoa wa Dar es Salaam haikuwa bora, hali iliyochangia kutokea mafuriko hasa msimu wa mvua.

Baadhi ya maeneo barabara zake ziliharibika, hapakuwapo mitaro ya kupitisha maji, mipangilio ya barabara na mitaa ilikaa vibaya.

Kuna mitaa haikuwa na taa, hapakuwapo masoko ya kisasa, hata kuchangia kukosekana mwonekano mzuri.

Hadi sasa, jitihada zimeshafanyika kwa kushirikiana na serikali na wadau wa maendeleo, kuupanga mji mkuu huo wa biashara nchini, kupitia Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP), uliohusisha maboresho ya miundombinu kwa wilaya tatu za Dar es Salaam; Temeke, Kinodoni na Ilala.

Miundombinu ikaboreshwa kwa kujenga barabara mpya zenye viwango lami, mifereji, madaraja, masoko, stendi za mabasi, viwanja vya michezo, vituo vya afya, sehemu za kupumzika, ujenzi wa vyuo vya umma na ununuzi wa magari ya kubeba taka.



Shughuli za kuchimba mifereji zilipokuwa zikiendelea, Tandale Mtogole, Dar es Salaam.

**MAPINDUZI YALIVYO**

Ni mradi uliogharimu Sh. bilioni 600 kutoka Benki ya Dunia, hata kufanya kuwapo maeneo thamani yake sasa imepanda, kodi za makazi na viwanja kuuzwa bei kubwa.

Mhandisi wa Mradi, Celestina Rugeyasila, anasema miaka 10 sasa mradi DMDP umedumu na maboresho makubwa, hususani barabara, kujenga madaraja katika maeneo yaliyosababisha mafuriko na watu wakashindwa kuvuka, mvua zinaponyesha.

Anasema DMDP imetumia mabilioni ya fedha kuondoa changamoto zilizokabili maeneo yao ya makazi, akisema wilayani Ilala, mradi umegharimu Sh. bilioni 120 na zilizosaidia kutatua changamoto zilizowatesa awali.

"Wananchi tunawaomba kama tulivyowashirikisha tangu mwanzo katika kuchagua hii miradi. Tumechagua sisi wenyewe tunatakiwa kuwa walinzi wa hii miradi tusikubali ikaharibiwa," anasema Rugeyasila.

Anasema kati ya Sh. bilioni 600 zilitolewa kwa ajili ya mradi wa mkoa wa Dar es Salaam, Manispaa ya Ilala walipatiwa Sh. bilioni 120 walizotengeneza barabara za lami kilomita 41, masoko matatu, kununua magari matano ya taka na kontena 15 za kuhifadhi uchafu.

Pia, anasema wametengeneza visima vya maji 10, stendi ya daladala yenye uwezo wa kuingia magari 70, vyoo vya umma vitatu na maeneo ya kupumzika, ikiwemo Mnazi Mmoja.

"Kuna madaraja ambayo hayakuwa katika mradi. Kutokana na mvua zilizonyesha mwaka 2018, daraja lilichukuliwa na maji, ikaonekana hatuwezi kutengeneza barabara nzuri, bila kuwa na daraja. Sehemu mbili ziligawanyika, mvua ikitokea watu hawawezi kurudi nyumbani," anaeleza Rugeyasila.

Anasimulia kwamba, iliwalazimu wananchi kutafuta maeneo ya kujihifadhi, baada ya kushindwa kurudi nyumbani na vifo vikatokea wakati huo, baadhi wakivushwa kwa kubebwa mgongoni, pia mikokoteni.

Rugeyasila anausifu mradi kutatua baadhi ya changamoto, hivyo anawataka wananchi waitunze, akionya wanaoharibu, wachukuliwe hatua.

**TEMEKE WAFURAHIA TAA**

Kaimu Mratibu Msaidizi wa DMDP Wilaya ya Temeke, Adelhard Kweyamba, anasifu mradi kuisaidia Manispaa Temeke na wananchi katika matatizo mengi, ikiwamo kupunguza mafuriko, kuimarisha usalama na kupatikana huduma za afya kwa wakati.

Anasema miradi hiyo wilayani Temeke, imegharimu Sh. Bilioni 213 na mpaka sasa wameshalipa Sh. bilioni 197, ambazo zimesaidia wananchi kupata barabara zenye kiwango cha lami kilomita 96 na nyingine zina zege.

Anataja miradi hiyo ni: Masoko sita, kati yake matano yamekamilika, lililobaki lilitarajiwa kukamilika mwezi uliopita; vituo vitatu vya mabasi, viwili vimeshakamilika na kilichobaki katika eneo Buza, inatarajiwa kukamilishwa karibuni.

Kweyamba anasema, mradi una mifereji urefu wa kilomita 15 inayopita kwenye makazi ya watu kupunguza tatizo la mafuriko.

Lingine analitaja ni kuwapo kituo cha kukusanya maji, karibu na Shule ya Sekondari Kibasila, Chang'ombe, Dar es Salaam.

"Mvua zilivyokuwa zinanyesha shule kama ya Kibasila walikuwa hawawezi kuingia madarasani. Tangu tujenge, inakusanya maji na kuyatoa kwa utaratibu na kuyapeleka baharini," anasema.

Lingine analitaja wamenunua magari 20 na makontena 65 kwa ajili ya kazi ya kukusanya na kusafirisha taka kwenda kwenye dampo lililopo, eneo la Pugu.



Kazi ya ujenzi wa barabara Sinza – Manzese, Dar es Salaam.
**PICHA ZOTE: MTANDAO.**

"Hii mifereji tuliyoiweka, imesaidia kupunguza mafuriko kwa kiwango kikubwa na ukiangalia barabara zetu nyingi tumeweka taa barabarani, ambazo katika jamii zetu zimeongeza ulinzi, ukabaji umepungua na wananchi wameongeza muda wa kufanya biashara zao," anasema.

Kweyamba anaeleza mradi ulijikita kwenye maboresho ya makazi ya wananchi wenye kipato cha chini, hivyo wanavyopita na vifaa vyao wakapata changamoto.

"Nyumba hazipo katika ubora wakati mwingine zina ufa tunapoweka mradi ufa unaongezeka, lakini tulijitahidi kuwarekebishia ili tuwaache katika mazingira mazuri," anasema.

**DMPD AWAMU II**

Kweyamba anasema, DMDP awamu ya Pili iko mbioni kuanza, ikitarajiwa kuwa na barabara nyingi zaidi, akiwaomba wananchi kuwa walinzi wa kutoa taarifa, wanapoona kuna hujuma.

Meneja Masoko wa Manispaa Temeke, Anzameni Mandari anasema mradi umewapa nafuu kiutendaji kuwa na masoko ya kisasa, kwani awali yalikuwa katika hali mbaya.

Mratibu DMDP Wilaya ya Kinondoni, Mhandisi Mkelewe Tungaraza, anasema walikutana na changamoto nyingi katika utekelezaji na ukawaongezea gharama, wakiwa wamelipa fidia ya zaidi ya Sh bilioni 17 kwa wananchi na mradi huo ulioanza mwaka 2016 hadi 2022 ukigharimu Sh. bilioni 215.9 wilayani humo.

"Tumewalipa hizo fedha ili tuweke miundombinu ya ujenzi unaweza, kuangalia hii fedha tungeweza kuiweka katika miundombinu tungeongeza kilomita kadhaa za barabara na kutatua changamoto ya usafiri," anasema.

"Kwenye maeneo ambayo ni njia za maji, tulikutana na malalamiko ya wananchi kudai nyumba zao zimechukuliwa na maji, tunataka kutekeleza mradi, mwananchi anadai nyumba yake na kutaka kulipwa fidia wakati sisi nyumba hatujaikuta," anaeleza.

Tungaraza anataja maeneo changamoto hizo zimejitokeza ni kwenye Mto Sinza, baadhi ya nyumba zimeondolewa na mafuriko kabla ya utekelezaji mradi, wakati ambapo maeneo hayo yalishazuiliwa kufanyika ujenzi.

Anasema wamefanikiwa kukabili adha hiyo, kwa kutengeneza mifereji inayookoa nyumba zisipate athari.

Katika maeneo yaliyopimwa, penye hifadhi ya barabara, Tungaraza anasema, kulisababisha kuchelewa utekelezaji wa mradi, kwani walilazimka kufufua mipaka ya viwanja vya wavamizi, kutambua uhalali na kasoro, kisha wakosaji wanawekewa ala za kuzibomoa.

Anataja changamoto nyingine, ni wananchi kutiririsha majitaka ndani ya mto Ng'ombe, pia kutupa taka ngumu.

"Taka ngumu zinaweza kusababisha madaraja kuziba, yakiziba baadaye tutapata changamoto za mafuriko ambayo hatukuyatarajia.

"Pia wapo baadhi ya watu ambao huiba yale mawe meusi tuliyoyaweka pembeni mwa mto ambayo hayapatikani Dar es Salaam, wanakuja kuyachukua na kutengeneza kokoto," anaeleza, akitahadharisha mkono wa sheria unawafuatilia wakosaji.

"Hivi sasa katika maeneo ambayo mradi umetekelezwa mwananchi anayetumia barabara anaweza kutumia njia mbalimbali kutoka eneo moja kwenda jingine, bila ya kukutana na changamoto, ikilinganishwa na awali kabla ya mradi kuanza,"anasema.

Tungaraza anasema, mradi huo ulihusisha kujenga barabara za lami na zege na kusimika taa hasa katika maeneo ya Mwananyamaka Bwawani, Tandale, Sinza, Kilongawima na Mbweni.

MAZINGIRA

# Migogoro isiyoisha ya ardhi, wizara yajibu na mradi wa Benki ya Dunia

## •Wizara Ardhi: Mkoa Pwani mfano wa shida sugu

**Na Julieth Mkireri, Kibaha**

SEKTA ya ardhi ni eneo ambalo kwa muda mrefu linakabiliwa na migogoro katika mipaka ya vijiji, viwanja, matumizi na umiliki. Hadi sasa kuna mrundikano wa kesi katika mabaraza ya ardhi.

Utapeli na kughushi nyaraka, ni kati ya vikwazo katika sekta ya ardhi, vimekuwa vikisababisha kutokuelewana kati ya jamii moja na nyingine, hata kukosekana maendeleo ya jamii kwenye maeneo yao.

Mkoa wa Pwani ni sehemu mojawapo ambako migogoro imesheheni, ikiwamo maeneo; Kibaha, Bagamoyo eneo la Mapinga na katika Halmashauri ya Chalinze.

Hapo na kwingineko mkoani Pwani, migogoro yake imejikita kwenye uvamizi wa maeneo yenye hati miliki, msuguano kati ya wakulima na wafugaji kuingiliana kwenye maeneo ambayo tayari ina mipango ya matumizi tofauti kisheria.

Kinachotokea, baadhi ya wananchi wamekuwa wakivamia maeneo yenye hati miliki na kujigawia, bila kufuata sheria na kanuni, huku wakiwatupia lawama wamiliki kwamba wameyatelekeza kwa muda mrefu, pasipo kuyaendeleza.

Pia, kuna kundi la matapeli wanaojivika kazi za udalali, wamekuwa wakiyauza maeneo hayo na kuchangia kuwapo migogoro isiyoisha.

Kikwazo kingine kinatajwa, ni cha eneo la mazingira na jamii kuwapo wanawake wachache wanaomiliki ardhi na ushirikishwaji duni wa wadau, hasa jamii za kifugaji na makundi maalumu.

### HATUA YA KISERIKALI

Kukithiri kwa hali hiyo kumeifanya serikali kutafuta fedha kutoka Benki ya Dunia, kuandaa mradi wa kumaliza shida hiyo, ikilenga usalama wa milki za ardhi, utekelezaji wake miaka mitano kuanzia Mei mwaka jana, ukitarajiwa kukamilika Mei 2027.

Mratibu wa mradi huo, Joseph Shewiyo, kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, anasema utekelezaji wa mradi huo, pia utaongeza uelewa na usalama wa ardhi, kwa kuzingatia nafasi ya jinsia na kuongeza idadi ya Watanzania wanaomiliki nyaraka za umiliki, huku wakipunguza muda unaotumika kupata nyaraka hizo.



Mbunge wa Chalinze, Ridhiwan Kikwete akikagua mipaka, akiambatana na baadhi ya viongozi wa kijiji cha Kwamduma, Chalinze mwaka 2018.

Shewiyo anataja mambo mengine ni katika malengo yake mahusus i, kwenda sambamba na kuongeza idadi ya miamala itokanayo na nyaraka za umiliki, iendane na ufanisi katika uandaaji wa nyaraka hizo.

Shewiyo anataja maeneo ya mjini wanakotekeleza hilo ni katika halmashauri za; Jiji Dodoma, Chalinze, Mafinga, Rungwe, Korogwe, Tarime, Nzega, Kigoma Ujiji, Kibaha Mjini, Bariadi, Iringa, Tanga, Tabora na Geita.

Pia, anataja halmashauri za; Shinyanga, Kahama, Jiji la Mbeya, Moshi, Kondoa, Bagamoyo, Kilolo, Kaliua, Bukombe, Musoma, Kishapu na Wilaya ya Moshi.

Hilo linaendana na mradi katika maeneo ya vijijini, anakokutaja kuwa ni Mbinga, Tanganyika, Songwe, Chamwino, Maswa, Mufindi na Longido.

### KAZI ZITAKAZOFANYIKA

Akizungumzia kuhusiana kazi zitakazofanyika katika mradi huo, ni utoaji wa hatimiliki milioni mbili katika maeneo ya mjini.

"Tutatumia asilimia 20 ya watumishi wa serikali na kampuni zilizosajiliwa zitafanya kazi za kupanga na kupima kwa asilimia 80 na kazi ya mfano imeanza katika jiji la Dodoma na kata tatu zimechaguliwa" anaeleza.

Shewiyo anasema, kuna halmashauri nane zinaanza kwa mwaka wa kwanza wa mradi ambazo ni Dodoma Jiji, Chalinze, Mafinga, Rungwe, Nzega, Tarime, Korogwe na Kigoma Ujiji.

Anagusia pia kutatolewa hatimiliki za kimila 20,000, kazi inayofanywa na watumishi wa serikali na taasisi zisizo za kiserikali, akitaja kazi zitakazofanyika katika maeneo hayo ya vijijini, ni, kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya sita.

Mratibu huyo wa Ardhi, anasema kuna jumla ya vijiji 250 vitakavyopimwa mipaka yao, pia mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 250, ikiandaliwa mipango ya kina katika vitovu vya vijiji tajwa.

Anaeleza kuwapo maandalizi ya ramani za msingi itakayofanyika, kwani ramani zilizopo sasa ziliandaliwa zama za miaka ya 1990, ikiwamo wastani wa miaka 30 sasa, hivyo zinahitaji maboresho, kazi itakayofanywa kwa uwezo wa ndani ya nchi.

Anasema, uboreshaji wa alama za msingi, pia utafanyika kwa kusambazwa maeneo ya mradi, ili kuongeza ufanisi wa upangaji na upimaji nchini.

### MIRADI INAVYOBORESHA

"Uboreshaji wa mfumo wa ILMIS utafanyika ili uweze kutumika nchi nzima baada ya kujaribiwa mikoa ya Dar es Salam na Dodoma," anasema.

Ni mradi utakaokaribisha ujenzi wa ofisi za ardhi mikoa 25, ukarabati wa ofisi ardhi katika halmashauri 41, kukarabati masijala ardhi za vijiji 250, kujenga jengo la kumbukumbu za ardhi nchini na madarasa makubwa mawili.

Anasema, mradi huo pia una utaratibu wa kuandaa nyaraka mbalimbali na utekelezaji wa usimamizi wa mazingira na masuala ya kijamii, pia utafiti na kuandaa miradi.



Aliyekuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Ridhiwani Kikwete, akizungumza kwenye moja ya mikutano yake kuhusu ardhi, katika Halmashauri ya Chalinze. **PICHA: JULIETH MKIRERI.**

Kwa mujibu wa Shewiyo, inayaangalia pia kuwezesha wanawake na haki za ardhi, pia ushiriki wao kwenye masuala ya kukabili ukatili na unyanyasaji wa kijinsia.

Mratibu anataja eneo lingine la kutekeleza malengo ya mradi ni mifumo ya utawala wa ardhi, ili kupunguza gharama na muda wa upatikanaji wake, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, huku kukipunguzwa kasi ya ukuaji wa makazi holela.

### NAIBU WAZIRI RIDHIWANI

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, anasema ni mradi unaoelekea kumaliza migogoro ya ardhi, inayojitokeza kila mara.

Ridhiwani, ambaye pia ni Mbunge wa Chalinze, anasema serikali imetambua uwapo wa migogoro isiyoisha katika maeneo mbalimbali nchini, hivyo imefikia hatua ya kutenga kiasi Sh. bilioni 345 za kupima ardhi nchini.

Anasema, katika hatua ya awali kuna halmashauri 41 nchini ikiwamo Chalinze, akiahidi suluhisho la migogoro kati ya kata, pia vijiji, hata inakwamisha maendeleo ya kijamii.

"Tunakwenda kutambua maeneo ya wakulima na wafugaji na katika hili, shughuli ya upimaji itafanywa na wenyeji kwa kuwahusisha vijana katika upimaji huo, huku wazee nao wakipewa nafasi kutokana na kuwa na historia za mipaka kwenye vijiji vyao," anasema.

Naibu Waziri huyo anayetumikia sasa nafasi hiyo katika Ofisi ya Rais (Utawala Bora), akaahidi Wizara ya Ardhi kuwaletea wataalamu kuwapimia, kisha vijana watapewa mafunzo kwenye kazi hiyo, vikitumika vifaa vya kisasa.

"Mkichukua watu ambao sio wenyeji kwenye eneo husika, mtasababisha migogoro, kwa maana watakuwa hawajui vizuri eneo hilo. Zingatieni kutoa kipaumbele kwa vijana wa eneo husika, ambao wataambatana na wataalamu kufanikisha kazi hii na kumaliza migogoro kwenye maeneo yetu.

"Rais Samia Suluhu Hassan amechoshwa na migogoro ya ardhi, ameamua kufikia hatua hii kutenga fedha kwa ajili ya kupima maeneo yetu, kila mtu atapimiwa eneo lake na kila kijiji na kata watapimiwa kujua mipaka yao na baada ya hapo kutatengenezwa ramani," anasema.

Anasema kumekuwapo migogoro mingi ikiwemo ya wakulima na wafugaji na mipaka na ili kuondoa migogoro hiyo ni kupima ardhi jambo ambalo serikali iko mbioni kulifanya.

Ridhiwani anakiri Chalinze ni kati ya halmashauri zenye migogoro ya ardhi lukuki.





# DC aonya matumizi chandarua kulimia mchicha, kufugia kuku

**Na Mwandishi Wetu**, DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Mwema, amekemea tabia ya wananchi wanaotumia vyandarua kulimia mchicha pamoja na kufugia kuku.

Alitoa karipio hilo juzi wakati wa ugawaji wa vyandarua vilivyowekwa dawa kwa wanafunzi wa shule za msingi za serikali na binafsi mkoani Dodoma.

Ugawaji huo ulifanyika katika shule ya msingi za Wilaya ya Chamwino iliyofanyika Shule ya Msingi Buigiri.

Alisema lengo la kutoa vyandarua ni kuwalinda wanafunzi dhidi ya ugonjwa wa malaria na sio kulimia mchicha.

Alisema dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha angalau kila mwanafunzi mmoja apate chandarua chake.

"Vyandarua hivi vinawalenga nyinyi wenyewe nataka nitume ujumbe kwenu usije ukachukua chandarua ukaenda nyumbani ukaenda kumpa mzazi kwamba tumepewa tukuletee." Alisema na kuongeza:

"Ninafahamu yamekuwa matumizi mengine mnaenda kutumia kulimia mchicha au bustani nataka niseme hapana, nasema hapana siyo matumizi sahihi semeni hapana,"alisema Mwema.

Hivyo, aliwataka viongozi wanaohusika na ugawaji kusimamia kikamilifu ili kuwafikia walengwa na siyo watu wengine.

Alisema: "Tunahitaji watoto wetu muwe na afya njema, ukiwa na afya njema utaweza kutimiza ndoto zako serikali inawapenda ndiyo maana jitihada zimechukuliwa."

Alisema wanahitaji kila mwanafunzi atambue umuhimu wa kutunza afya.

"Nendeni mkawaambie wazazi wenu, majirani kwamba vyandarua hivi haviuzi na yeyote atakayeuza atachukuliwa hatua kali za kisheria, imani yangu mnaenda kufanya matumizi sahihi," alisema.

Alibainisha mpaka sasa wilaya hiyo imepokea vyandarua 17,556 kwa wanafunzi zaidi ya 88,000.

Meneja Kanda wa Bohari ya Dawa (MSD) Dodoma, John Sipendi, alisema wamezindua usambazaji wa vyandarua katika shule za Wilaya ya Chamwino kwa uratibu na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ( TAMISEMI).

Alisema kwa Mkoa wa Dodoma wanatarajia kusambaza zaidi ya vyandarua 560,000 ambavyo watazifikia shule 862.

Alisema: "Niwatake wanafunzi waendelee kutumia kwa malengo yaliyokusudiwa lengo ni kuzuia maambukizi yafikie asilimia sifuri kwani kwa Wilaya ya Chamwino kuna maambukizi asilimia 0.7".

# DUWASA kujenga mtandao wa uondoshaji majitaka

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi na Mazingira Dodoma (DUWASA) inapanga kujenga mtandao wa uondoshaji majitaka wenye urefu wa kilomita 250 utakaogharibu Sh. bilioni 161.

Mkurungenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, alisema hayo jana wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari akielezea mafanikio na majukumu ya mamlaka hiyo.

Alisema DUWASA inakusudia kujenga kilomita 250 za mtandao wa majitaka wa Sh. bilioni 161 ili kukabiliana na ongezeko la watu kuhamia jijini hapo.

Aidha, alisema gharama hizo zinahusisha ujenzi wa mtandao wa majisafi wenye kilomita 8.5 na majitaka kilomita 52 katika mji wa serikali Mtumba.

Pia alisema fedha hizo zitahusisha ujenzi wa mabwawa ya kutibia majitaka eneo la Chang'ombe Buigiri wilayani Chamwino.

Alisema mhandisi ameshafanya mapitio ya usanifu na kuwasilisha mpango wa mradi huo.

Kadhalika, alisema fedha hizo zitaelekezwa kusaidia ujenzi wa mradi huo wa maji taka kwenye maeneo mengine ya Jiji hilo. Aidha, alisema katika kukabiliana na ongezeko hilo serikali kupitia Wizara ya Maji na DUWASA imewekeza Sh. bilioni 9.14 kwa hatua za muda mfupi za kupunguza tatizo la maji.

Alisema fedha hizo zitatumika uchimbaji na uendelezaji wa visima 32 sehemu mbalimbali za huduma, ufungaji wa pampu pamoja na ulazaji wa mabomba ya majisafi.

Aliongeza kuwa ujenzi huo utakuwa ni kilomita 208.86 za mtandao wa kusafirishia na kusambazia maji, ujenzi wa matangi yenye ujazo wa lita 3,035,000.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema mkoa unakusudia kufikisha huduma muhimu kwa wananchi ili kupunguza malalamiko.

Senyamule alisema kuna mabwawa makubwa mawili yanajengwa ili kukabiliana na tatizo la maji kwenye maeneo Wilaya ya Chamwino na Mpwapwa.

Hata hivyo alisema mabwawa hayo yatatumika kwa ajili ya maji ya kunywa na kusaidia kwenye kilimo cha umwagiliaji.



Iliyokuwa stendi ya daladala ya Sabasaba jijini Dodoma ikionekana kuwa wazi baada ya kuondolewa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kuanzia jana na kuihamishia kituo kipya cha soko la Machinga eneo la Bahi Road. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wafanyabiashara Soko la Sabasaba wagoma kuondoka kupisha ujenzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFANYABIASHARA zaidi ya 3,000 wa Soko la Sabasaba jijini Dodoma wamegoma kuondoka katika eneo hilo kupisha ukarabati ambao unapangwa kufanywa na halmashauri ya Jiji hilo.

Wamesema endapo wataendelea kusumbuliwa watasitisha huduma na kufanya maandamano kwenda Ikulu kumwona Rais Samia Suluhu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika mkutano wa hadhara juzi walidai kuwa uongozi wa Jiji umekuwa ukiwasumbua kila siku kuwataka kuondoka bila kuushirikisha.

Makamu Mwenyekiti wa Soko la Sabasaba, Kombo Kombo, alisema wameamua kuitisha mkutano huo kutokana na maagizo ya mara kwa mara ambayo yamekuwa yakitolewa na uongozi wa Jiji kuhusu kuondolewa kwao.

"Hapa sisi wafanyabiashara maazimio yetu ni hakuna mtu ambaye ataondoka kwani hapa sisi tumewekeza na tunalipa kodi na leseni tunazo na tulikuja hapa kwa mujibu wa sheria hakuna mtu aliyevamia tupo hapa toka utawala wa Rais Hayati Benjamin Mkapa,"alisema. Alisema hivi karibuni uongozi wa Jiji ulipitisha tangazo kupitia gari la matangazo ukiwataka wafanyabiashara wote kwenda kuhakikiwa katika ofisi ya Jiji. "Hakuna mtu kwenda kuhakikiwa kule Jiji kama wanataka waje hapa kwani hizi ndiyo ofisi za wafanyabiashara, lakini wenzetu wa upande wa magari tayari wameshaambiwa wanatakiwa kuondoka hapa katika Stendi ya Sabasaba Machi Mosi mwaka huu ili kuhamia Soko la Machinga,"alisema Kombo.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Tausi Rajabu, alisema wanamwomba Rais Samia kuwaonea huruma kinamama ambao wamekopa mikopo lakini kutokana na usumbufu wanaupata wanashindwa kufanya biashara na kurejesha kwa wakati.

"Soko hili hivi sasa Jiji wanalitamani kutaka kujenga maghorofa lakini sisi ndiyo tumelifanya lionekanane hivi lilikuwa chafu lakini leo tumeliboresha kwa gharama zetu wenyewe wao hakuna hata Sh. 10 yao hapa ndiyo maana leo hii wanadai kutaka kujenga ghorofa na kutuondoa sisi kama wanalitamani waje tukubalianae tuwauzie,"alisema Rajabu.

Mfanyabiashara mwingine, Joseph Mazengo, alisema wao ni Watanzania na wataendelea kutumia soko hilo na hakuna hata mmoja wao ambaye ataondoka kwani Jiji wamekuwa wababaishaji kwa kuweka mipango ambayo imekuwa ikiwagharimu wao.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alipotafutwa kutolea ufafanuzi kuhusu malalamiko hayo alisema suala la kuhamishwa stendi ya daladala katika soko hilo siyo maamuzi yake bali watafutwe LATRA ndiyo watakuwa na majibu.





# RC aunda kikosi kupambana wanaovuna majani mabichi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ametangaza kuunda kikosi maalum cha kushughulikia kampuni na wakulima wanaovuna majani mabichi ya pareto.

Amesema watu hao wanasababisha bidhaa zinazozalisha ikiwamo viuatilifu kutokuwa na ubora unaotakiwa.

Homera alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari juu ya msimamo wa serikali katika kuboresha pareto ambayo kwa kiasi kikubwa inalimwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Alisema kwa sasa anaunda tume ya kusimamia watu wote watakaovuna zao hilo likiwa bado halijakomaa ili wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria na kuwa fundisho kwa wengine.

"Kuna vikwazo vikubwa sana katika pareto, wapo wafanyabiashara ambao siyo waaminifu wanavuna maua mabichi hali inayosababisha hasara kubwa kwa bidhaa zinazotengenezwa, nimeagiza kuanzishwa kwa operesheni maalum ya kushughulikia wakulima na wafanyabiashara wanaovuna majani mabichi kwa sababu wanasababisha hasara ya bidhaa zinazozalishwa,"alisema Homera. Alibainisha hasara zinazotokana na uchumaji wa maua mabichi ya pareto ambayo yanapelekwa viwandani kuwa ni kusababisha madhara ya kiafya kwa watuamiaji, bidhaa zao kutokuwa na soko kwa sababu hazijakidhi vigezo vinavyohitajika.

Akizungumzia suala hilo, Mdhibiti Ubora wa pareto mikoa ya nyanda za juu kusini, kutoka Bodi ya Pareto (TPB), Edwin Margwe, alisema tayari wamepokea malalamiko hayo na kwamba wanatarajia kukutana na wadau mbalimbali wa zao hilo ili kujadili vikwazo vinavyosababisha uchumaji wa maua mabichi ya pareto.

"Tumekuwa na utaratibu wa ukaguzi wa zao hili mara kwa mara ambapo tunatembelea maghala ya kuhifadhia na vituo vinavyonunua lakini hatujawahi kuona maua mabichi, tumepokea taarifa kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera kwamba wapo baadhi ya wakulima na makampuni yanayonunua maua mabichi, bodi tutakaa na kufanya maamuzi ya kukomesha suala hilo," alisema Margwe.

Aidha alisema Wilaya ya Mbeya ndiyo inayotegemewa nchini kwa uzalishaji mkubwa wa pareto ambapo kwa mwaka hukusanya tani kati ya 1,500 hadi 2,000.

Alisema licha ya uzalishaji huo kwa mwaka lakini msimu huu wanatarajia kukusanya zaidi hadi tani 3,000 za pareto kutokana na hali ya hewa kuwa nzuri mwaka huu.

Akizungumzia upatikanaji wa soko la zao hilo, alisema upo kwa asilimia 100 kutokana na uwapo wa kampuni saba ambazo zinasubiri mazao kutoka kwa wakulima.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Simon Mayeka, akiijaribu moja ya pikipiki kati ya 33 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kuwawezesha maofisa ugani na kilimo wilayani humo jana kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# DC awapa hadhari wakulima wanaovuna parachichi mbichi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKULIMA wa parachichi Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya wameshauriwa kuacha kuvuna na kuuza parachichi ambazo hazijakomaa kwa kuwa kufanya hivyo wanaharibu soko la zao hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu alitoa ushauri huo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Busokelo ambapo aliwataka madiwani kuwaelimisha wananchi hasara za kuvuna na kuuza parachichi ambazo hazijakomaa.

Wenzetu wa kilimo wanajitahidi sana kutafuta kampuni za ununuzi lakini baadhi ya wanunuzi wamekuwa siyo waaminifu wanakuja kununua parachichi ambazo hazijakomaa wanapeleka sokoni, hivyo kwenye soko tunaonekana kutoka rungwe tunapeleka parachichi ambazo hazijakomaa,"alisema Haniu. Alisema jambo hilo linaharibu soko kwani wanunuzi wengine wataacha kununua parachichi hizo kwa kuhofia kwamba hazijakomaa na kwamba itawaharibia soko la ndani na nje na kuwakosesha wakulima na halmashauri kipato.

"Taarifa zikifika kule kwamba parachichi zinazouzwa Rungwe hazijakomaa hii itawakimbiza wanunuzi na makampuni haya hatutayapata, hivyo naomba tulisimamie hili na msimu huu wa ununuzi unapoanza pia tusimamie bei elekezi na wakulima walipwe kwa wakati," alisema.

Baadhi ya madiwani walisema wapo wakulima katika baadhi ya vijiji wanalima parachichi kwa wingi lakini wanakosa masoko kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara na kuiomba serikali kujenga barabara katika maeneo hayo ili kurahisisha shughuli za kibiashara.

Diwani wa Kata ya Lufilo, Lucus Mwamafupa alisema: "Wakulima kule Kabembe wamelima sana parachichi unakuta mtu mmoja amelima zaidi ya ekari 20, lakini walikolima hakuna barabara tunaomba Serikali itujengee barabara ili wakulima wapate kipato lakini pia halmashauri itapata ushuru".

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Busokelo Rungwe, Hawa Hassan alisema kwa sasa hakuna changamoto ya masoko kwa zao hilo katika halmashauri hiyo kwani wanunuzi kutoka kampuni mbalimbali wanafika kununua bidhaa hiyo.

# Daktari awatoa hofu walaji nyama ya nguruwe

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

DAKTARI wa mifugo Mkoa wa Mbeya, Dk. Samora Mshani, amewatoa hofu wananchi wa mkoa huo kuwa ugonjwa wa homa ya nguruwe hauna madhara yoyote kwa binadamu.

Amesema hata mtu akila nyama ya nguruwe mwenye ugonjwa huo hatapata athari yoyote.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na Nipashe baada ya kuenea kwa uvumi kwamba mtu atakayekula nyama ya nguruwe aliyeumwa atapata madhara ya kiafya.

Alisema nguruwe aliyeugua ugonjwa huo anakufa ndani ya kipindi kifupi na nyama yake ni nzuri na inaweza ikaliwa na binadamu na hatapata madhara yoyote kwa sababu ugonjwa huo hauambukizwi kwa binadamu.

Alifafanua kuwa homa ya nguruwe inaenezwa na virusi na haina tiba na kwamba baadhi ya watu wanasisitiza nguruwe mwenye ugonjwa asiliwe kwa sababu ya usafirishaji wa nyama hiyo kwenda eneo lingine unaweza kueneza ugonjwa huo kwa nguruwe wengine.

Alisema ili kuthibiti ugonjwa huo wafugaji wanapaswa kuwapa nguruwe chakula cha kutosha, kuzingatia usafi wa mabanda, kuhakikisha nguruwe wote wanafanyiwa ukaguzi wa kitaalamu pamoja na kuhakikisha nguruwe waliopata ugonjwa wanafukiwa kwenye shimo refu au wanachomwa moto.

"Ugonjwa huo upo nchini kwa muda mrefu lakini huzuka kwa kasi zaidi kipindi cha masika kwa sababu ya uwezekano wa kusambaa kwa sababu ya maji kuwa mengi ni mkubwa," alisema Dk. Mshani.,

Hivyo, aliwataka wananchi kutokuwa na hofu ya ulaji kitoweo hicho kwa sababu binadamu akila nyama ya nguruwe hapati ugonjwa wowote ule na kwamba wafugaji wanapaswa kuchukua tahadhari zinazotolewa ili kuepuka hasara.



# Majaliwa: Wabunge wanawajibu wa kuishauri serikali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema wabunge wanawajibu wa kuishauri serikali katika harakati za kuleta maendeleo kwa wananchi.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya wajumbe wa kamati ya uongozi na makamu wenyeviti wa kamati za kudumu za Bunge katika ofisi za Bunge Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema katika kufikia maendeleo ya wananchi kupitia Bunge watendaji wa Bunge wanatakiwa kufanya kazi zao kwa uweledi katika kuishauri serikali mipango ya maendeleo.

Majaliwa alisema Bunge ni moja ya mhimili wa serikali, hivyo wenyeviti wa kamati lazima wafanye kazi zao kwa mujibu wa sheria bila ya kuingilia mhimili wa serikali kwa kuwa mihimili hiyo kila mmoja inafanya kazi zake kwa mujibu wa utaratibu uliyowekwa.

Alisema mafunzo hayo ni muhimu na yatawajengea uwezo viongozi hao katika kufanyakazi zao katika Bunge pamoja na kuwatetea wananchi. Majaliwa alisema viongozi wa Bunge wanatakiwa kufahamu kuwa namna bora ya kuongoza na siyo kutumia madaraka yao vibaya kwani kwa kufanya hivyo ni kinyume na utaratibu na sheria za utumishi wa umma.

Aidha, alisema viongozi na wenyeviti wa Bunge wanatakiwa kuendelea kufahamu kuwa rushwa ni njia mojawapo ya kudhorotesha uchumi, hivyo kunakila sababu kwa wabunge na viongozi wengine kuwa mstari wa mbele katika kukemea suala la rushwa na uongozi usiofuata madili katika utendaji wa kazi za kila siku.

Majaliwa alisema mafunzo hayo ya uongozi yamekuja wakati muafaka kwa vile hivi karibuni Bunge litaanza vikao vya bajeti, hivyo wenyeviti hao watakuwa wawe vizuri katika kufanya kazi zao bila ya kuingilia mhimili mwingine.

Majaliwa alisema Bunge la bajeti litakuwa la kipindi kirefu katika kufanya kazi lakini watendaji hao watafanya kazi zao kwa kujiamini kwa kuwa mafunzo ya uongozi wameshapatiwa.

Alisema katika mada ambazo zitawasilishwa haiba ya viongozi na itifaki ya kidiplomasia katika utekelezaji wa shughuli za kibunge na kiserikali kwenye ngazi ya kitaifa na kimataifa, hivyo watumishi hao wanatakiwa kujua kila kitu juu ya jambo hilo.

Alisema wabunge pia wanapaswa kujua utaratibu na utekelezaji wa shughuli za serikali katika kamati za Bunge, mahusiano na changamoto ili kujitafakari juu ya utendaji wa kazi wakati wote wanapokuwapo bungeni.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alisema wameamua kuwapa mafunzo hayo wenyeviti ili kuona namna gani wanafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria bila ya kuingilia mhimili mwingine wa nchi.

Alisema watumishi hao wanawajibu wa kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria bila ya kuingilia mhimili mwingine wa serikali katika utendaji wa kazi zao wakati wote.



Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania ( TCD) na Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana (wa pili kushoto), akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa viongozi wa vyama vya siasa vya Tanzania na Burundi, ulioandaliwa na TCD, jijini Zanzibar juzi na kujadili umuhimu wa majadiliano baina ya vyama vya siasa. Wengine ni Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba (wa tatu kushoto) na (kulia) Kiongozi wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe. **PICHA: FAHADI SIRAJI WA CCM**

# SMZ yatangaza mwelekeo wa mpango wa maendeleo 2023-34

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetangaza mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023-2034 pamoja na bajeti ya serikali ambayo imejipanga kutekeleza miradi ya kimkakati ya ujenzi wa bandari shirikishi ya Mangapwani Unguja.

Pia imetangaza kujenga Kiwanda cha Ndege cha Pemba, kujenga miundombinu ya barabara za ndani ikiwamo za vijijini ambazo zitaimarisha mawasiliano ya usafiri na sekta ya utalii.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, DK. Saada Mkuya Salim, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiwasilisha mpango huo pamoja na bajeti kuu ya serikali ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema katika mpango huo kipaumbele ni kutekeleza miradi ya kimkakati ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa mwaka 2020-2025 pamoja na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar. Dk. Mkuya alisema katika mikakati ya kukifungua kisiwa cha Pemba, serikali imepanga kujenga Kiwanja cha Ndege cha Pemba ambapo maandalizi yote yamekamilika.

Alisema katika mpango huo ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Nungwi unatarajiwa kujengwa ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuongeza miundombinu ya usafirishaji na kukuza sekta ya utalii.

Alisema mradi wa ujenzi wa Bandari shirikishi ya Mangapwani unatarajiwa kujenga pamoja na bandari nyingine ikiwamo Malindi, Wete, pamoja na mkoani Pemba.

Aidha, alisema katika ujenzi wa miundombinu ya barabara serikali inakusudia kujenga barabara ya Chake-chake hadi Wete yenye urefu wa kilomita 22 ambayo inakwenda kukiunganisha Kisiwa cha Pemba na mikoa miwili.

Alisema ujenzi wa Barabara ya Tunguu hadi Makunduchi yenye urefu wa kilomita 48.5 itajengwa pamoja na Barabara ya Fumba hadi Kisauni Unguja yenye urefu wa kilomita 12.

Katika kuimarisha miundombinu ya barabara yenye lengo na kuimarisha sekta ya utalii, Dk. Mkuya alisema serikali inakusudia kujenga barabara za ndani kwenda vijijini zenye urefu wa kilomita 275.9 pamoja na ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 277.

Waziri Mkuya alisema mwelekeo wa bajeti kwa mwaka 2023-2024 yapo mambo mahususi yamezingatiwa ikiwamo ongezeko la pensheni jamii kwa wazee pamoja na pensheni kwa wastaafu.

Alieleza kuwa mwelekeo wa bajeti kwa mwaka 2023-20245 mapato ya serikali yanatarajiwa kufikia Sh. trilioni 2.7 ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 149.13 sawa na asilimia 16 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2022-2023 ya Sh. trilioni 2.5.

Alisema kati ya fedha hizo Sh. trilioni 1.4 zitakusanywa katika vyanzo mbalimbali vya mapato.

# Chanzo vifo vya mama na mtoto kuongezeka chatajwa

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema kuwa asilimia 30 ya wajawazito hawafiki katika vituo vya afya na hospitali hali inayochangia ongezeko la vifo vya mama na mtoto.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa mafunzo kwa wataalamu wa afya namna ya utumiaji wa bidhaa za kisasa kwa ajili ya usafishaji wa mimba kwa ajili ya kulinda afya za wanawake katika uzazi, mafunzo ambayo yameandaliwa na taasisi ya DKT Tanzania.

Alisema bado vifo vya mama na watoto Zanzibar ni tatizo hivyo lazima hatua madhubuti zichukuliwe katika kupunguza hali hiyo.

"Malengo ya dunia ifikapo mwaka 2030 tuweze kupunguza vifo chini ya 70 kwa watu laki moja, sisi tupo karibu 160 hivyo tunakazi kubwa ya kufanya ya kupunguza vifo vya mama na mtoto,"alisema Mazrui.

Alisema vifo hivyo vinatokana na sababu mbalimbali ikiwamo mjamzito kuchelewa kufika hospitali wakati wa kujifungua, lakini pia kutohudhuria kliniki kwa wakati.

Alisema hali hiyo inasababisha wanawake hao kutokwa na damu nyingi na wengine kupata saratani ya shingo ya kizazi kwa sababu hutoa mimba kwa njia zisizo sahihi na kukosa kusafishwa vizuri. Alisema bidhaa hizo zilizotolewa na Taasisi ya DKT, vitapunguza vifo vya mama na mtoto lakini kupunguza maumivu makali kwa mama wanaosafishwa baada ya mimba kuharibika.

Alisema wengi wao katika vituo vya afya wanatumia kifaa kijulikanacho kwa mdomo wa bata kwa ajili ya kusafisha mimba inapoharibika na kifaa hicho kinamadhara makubwa, hivyo ni vyema kuondokana na matumizi ya kifaa hicho ambacho kina maumivu makali. Naibu Mkurugenzi wa Kinga kutoka Wizara ya Afya, Fatma Kabola, alisema bado vifo vya watoto vipo na kwa wiki huwa na wastani wa vifo 10.

Alisema lengo la serikali ni kutokomeza vifo vya mama na mtoto na juhudi kubwa zinafanyika katika kuondoa vifo hivyo ikiwamo kuboresha huduma za afya.

Alisema idadi ya wasichana kuanzia miaka 16 hadi 25 wanaongoza kwa kutoa mimba kutokana na kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi wakiwa na umri mdogo. Mkuu wa Idara ya Masoko wa Taasisi ya DKT Tanzania, Deogratius Kitama, alisema bidhaa hizo ni kwa ajili ya kulinda afya za wanawake katika masuala ya uzazi na kuepusha vifo vitokanavyo na uzazi.

Alisema bado elimu inahitajika kwa jamii kuhusu uzazi salama na pindi mama mjamzito anapolazimika kutoa mimba ni lazima kuwapo na ushauri wa daktari na kutumia njia salama za utoaji wa mimba.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH (ELCT) KONDE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **PRADO** yenye usajili namba: **T498 BJC** . Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MBE/MBE/RB/78212/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PHILIP MBOBO JAYUNGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CALDINA** yenye usajili namba **T394C**KL, CHASSIS NAMBA: **AZT2410022953,** ENGINE NAMBA: **1AZ4982382.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI CONTROL NAMBA: **9910835458527/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SIMION WANGWE ERNEST** anatangaza kupotea kwa cheti cha Diploma in **Education at Open University Tanzania Adm** Na. **ND 2016986469** kilichotolewa mwaka 2020.Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA:**MAS/RB/2346/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOSES ELIYONA MEENA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 764 ANB – TOYOTA HILUX.** Chassis **No. YN670024368.** Engine **No. 4Y0247337.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/80814/2023.**

**Magistrates Court( Approved Forms For the Primary Court)**
**GN. NO 943(Contd.)**
**FOMU MIRATH -2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Morogoro**
**Kituo cha Mjini Mkoa Morogoro**
**Usimamizi wa mirathi Na 21 /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU GRACE WARIA MMARI WA AREA FIVE KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUWA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA NDUMINSARY WARIA MMARY**

### TANGAZO

**Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 Mwezi 03 Mwaka 2023 Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo,

**Zingatia :**

Endapo kuna mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na wawea kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia

**Imetolewa leo tarehe 23 Mwezi 02 Mwaka 2023**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO Mjini MOROGORO
..............................
**HAKIMU**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SALUM MUSSA NDEGE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 516 DRP – MITSUBISH CANTER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHA/RB/9084/2023**


## PATA MKOPO KWA HARAKA

PATA MKOPO KWA HARAKA
**HADI 200,000,000/=**
KUTOKA
**ENTERPRISE FINANCE LIMITED**
KWAAJILI YA DHARURA
MBALIMBALI KAMA KULIPA
KODI YA NYUMBA,
KUNUNUA GARI,
KUBORESHA BIASHARA N.K

**TUNAPATIKANA**
DAR ES SALAAM **0677111333**
NA ARUSHA **0677226960.**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MBEYA**
**KITUO CHA MBALIZI MKOA WA MBEYA**
**SHAURI LA MADAI Na 04/2009**
**Mdai la Madai BALONI NKWAMA**
**Jina la Mdaiwa**
**1.YOHANA MSOKWA.**
**2.ADMINISTRATOR GENERAL.**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA

**[Kanuni ya 18 ya kanuni za utaratibu wa Madai katika mahakama za mwanzo]**

**KWA;**
**1.YOHANA MSOKWA WA UYOLE MBEYA**
**Kwa kuwa Mdai /Wadai ameleta /wameleta madai yake /yao kwamba [Eleza hapa habari za Madai] JUU YA MADAI YALIYOLETWA MBELE YA MAHAKAMA.**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 17 mwezi 03 mwaka 2023 saa 2;30 asubuhi /mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO;Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 27 mwezi 02 mwaka 2023.


## OFISI ZA MATANGAZO

*Mikocheni Industial Area,*
*Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz*
*Website: www.ippmedia.com*

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais mteule Nigeria aomba mshikamano

**ABUJA, Nigeria**

BAADA ya kutangazwa mshindi katika uchaguzi mkuu wa Nigeria, Rais Mteule Bola Tinubu kutoka chama cha APC, ametetea uadilifu wa tume huru ya taifa ya uchaguzi na kutoa wito wa mshikamano.

Hata hivyo, vyama vya upinzani vimeutaja uchaguzi huo kuwa umejaa kasoro nyingi zinazoleta hofu.

Tinubu alitangazwa jana na mwenyekiti wa tume huru ya taifa ya uchaguzi ya Nigeria (INEC) Mahmood Yakubu, katika matokeo ya uchaguzi wa rais yaliyokuwa yakisubiriwa kwa shauku.

Mgombea huyo wa APC, ali HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/tinubu-mshindi-uchaguzi-wa-nigeria/a-64848547" jizolea jumla ya kura milioni 8.79 katika uchaguzi uliofanyika mwishoni mwa Juma, akiwa mbele ya mpinzani wake mkuu Atiku Abubakar, ambaye alipata kura milioni 6.98.

Peter Obi mgombea aliyepata umaarufu miongoni mwa vijana, wasomi na wapiga kura wa maeneo ya mijini ameibuka nafasi ya tatu kwa kupata kura milioni 6.1.

Kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi, mgombea anaweza kushinda uchaguzi wa Nigeria kwa kupata kura zaidi kuliko wapinzani asivuke chini ya asilimia 25 ya kura na kupata angalau theluthi mbili ya majimbo 36 na mji mkuu wa shirikisho Abuja.

Mara baada ya kutangazwa mshindi, Tinubu amewaeleza wafuasi wake kwamba amekabidhiwa majukumu makubwa na anayakubali.

"Ni nchi moja ambayo lazima tuijenge pamoja. Tunafanya kazi pamoja ili kuziba ufa uliojitokeza. Lazima tufanye kazi kwa ajili ya umoja, furaha na maelewano. Naahidi nitashirikiana nanyi kuifanya Nigeria kuwa nchi ya kurejea nyumbani ili kuchangia maendeleo ya nchi, " alisema Tinubu.

Uchaguzi wa Nigeria ulikuwa unatazamwa kuwa wa haki na wa wazi, lakini mchakato huo uligubikwa na hitilafu kadhaa kutokana na teknolojia mpya ambayo haikufanya kazi kama ilivyotarajiwa.

Tume ya uchaguzi iliahidi ingechapisha matokeo kutoka kila kituo cha kupigia kura kwenye tovuti yake kwa muda unaofaa, lakini vituo vingi vilishindwa kufanya hivyo na hivyo kutia dosari mchakato wenyewe.

Kutokana na kasoro hizo, wagombea wa vyama vya upinzani wakiongozwa na Atiku na Obi wameyakataa matokeo wakidai kuna udanganyifu.

Hata hivyo, Rais mteule Tinubu anakabiliwa na mlolongo wa matatizo kadhaa yanayolikumba taifa hilo, ikiwa ni pamoja na uasi wa wanamgambo wa Kiislamu wenye itikadi kali upande wa Kaskazini Mashariki, mashambulizi, mauaji, utekaji nyara, mzozo baina ya wafugaji na wakulima, uhaba wa mafuta, rushwa na ukosefu wa umeme.

Waangalizi wa kimataifa, wakiwemo kutoka Umoja wa Ulaya nao walibaini matatizo makubwa ya vifaa, wapiga kura kunyimwa haki na ukosefu wa uwazi wa tume ya uchaguzi.

Rais anayemaliza muda wake Muhammadu Buhari, pia kutoka chama cha APC alimpongeza mrithi wake akisema ni mtu sahihi kwa kazi hiyo na yuko tayari kufanya kazi pamoja ili kukabidhi madaraka kwa amani.

Tinubu mwenye umri wa miaka 70 na mwanasiasa mkongwe, alijipambanua kwa kauli mbiu iliyosema 'ni zamu yangu', ameahidi kurejesha matumaini mapya.

*DW*



Rais mteule wa Nigeria, Bola Tinubu akiwashukuru wananchi baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kumtangaza mshindi katika mji mkuu wa Abuja, juzi. **PICHA: AP**

# Vikosi vya Russia vyakaribia kuukamata mji wa Bakhmut

**KYIV, Ukraine**

VIKOSI vya Russia vimeendelea kusonga mbele katika operesheni yao ya kuuzingira na kuukamata mji wa Bakhmut ulioko mashariki mwa Ukraine.

Rais Volodymyr Zelenskiy, alisema juzi kwamba adui yao anaharibu kila kitu kinachoweza kutumiwa kulinda ngome zao.

Hata hivyo, Rais wa Russia, Vladmir Putin ameiagiza idara ya usalama ya (FSB) kuimarisha usalama katika majimbo manne yanayodhitibiwa.

Alisema katika sehemu hizo askari wake wapambane na kile alichokielezea kama ongezeko la operesheni za kijasusi na hujuma dhidi ya nchi yake zinazofanywa na Ukraine na nchi za Magharibi.

Aliyasema hayo baada ya gavana mmoja wa kikanda kusema ndege isiyo na rubani ilianguka karibu na kituo cha kusambaza gesi asilia, akidai ni shambulizi lililoshindikana karibu na mji wa Kolomna, kusini mashariki mwa Moscow.

Wakati huo huo, Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Marekani Antony Blinken, aliahidi msaada wa Marekani kwa nchi za Asia ya Kati ili kupunguza utegemezi wa kanda hiyo kwa Russia.

Kauli hiyo ameitoa siku chache baada ya kumbukumbu ya mwaka mmoja tangu uvamizi wa Russia,wakati alipokutana na mawaziri wenzake kutoka mataifa matano ya Asia ya Kati.

Akiwa katika mji mkuu wa Kazakhstan, Astana, Blinken ametangaza msaada wa dola milioni 25, kando na dola za awali milioni 25 zilizotangazwa Septemba, kuyasaidia mataifa ya Asia ya Kati kutanua njia za biashara na kutengeneza nafasi za kazi.

*DW*

# Ajali ya treni yaua 26 Ugiriki

**ATHENS, Ugiriki**

WATU 26 wamepoteza maisha na wengine kujeruhiwa baada ya treni mbili kugongana kaskazini mwa Ugiriki.

Baada ya ajali hiyo, waokoaji wameendelea kufanya kazi ya kuokoa abiria na kuzima moto uliosababishwa na ajali hiyo iliyotokea karibu na jiji la Larissa juzi jioni.

Ilielezwa treni hiyo ilikuwa na abiria 350, iligonga treni ya mizigo.

Video fupi zilizochapishwa kwenye tovuti za habari za nchini humo, zilionyesha miale ya moto mkali na moshi ukitanda kutoka kwa mabehewa yaliyoharibika.

Bado haijajulikana ni nini kilisababisha kugongana kwa treni hizo.

*BBC*

# Uganda kuongeza sheria kupambana na ushoga

**KAMPALA, Uganda**

Uganda imetangaza kuandaa muswada mpya wa kupinga vitendo vya mapenzi ya jinsia moja.

Kauli hiyo inakuja baada ya kuwepo kwa uvumi katika mitandao ya kijamii kuwa kuna makundi ya kimataifa ya kukuza ushoga yameingia nchini humo.

Spika wa bunge, Annet Among, katika akaunti yake ya Twitter, aliweka video akiwa katika mkutano wa maombi ya kidini na kisha aliandika kuwa Uganda italinda maadili na utamaduni wake kwa njia zote.

Serikali za Magharibi na mashirika ya misaada yanayofanya kazi nchini humo mara kwa mara yanatuhumiwa kuhimiza vitendo vya ushoga.

**Spika wa bunge, Annet Among, katika akaunti yake ya Twitter, aliweka video akiwa katika mkutano wa maombi ya kidini na kisha aliandika kuwa Uganda italinda maadili na utamaduni wake kwa njia zote.**

# YANGA YAANIKA MKAKATI WA MAKOMBE, ROBO FAINALI CAF

**Na Saada Akida**

HUKU wakiongoza mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara na wakati huo huo wakishika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Kundi D wa Kombe la Shirikisho Afrika, lakini wakiwa katika kinyang'anyiro cha Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, uongozi wa Klabu ya Yanga umesema dhamira yao msimu huu ni kuhakikisha wanafanya makubwa hususan michuano ya kimataifa na kuendelea kutetea mataji yaliyopo mbele.

Yanga kesho ina kibarua kigumu katika kuhakikisha inapata ushindi kwenye mchezo wao wa ASFC dhidi ya Tanzania Prisons utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Baada ya mchezo huo wa kesho, Yanga itaanza kujiandaa na mfupa mgumu mwingine Jumatano ya wiki ijayo dhidi ya Real Bamako ya Mali, ikiwa ni mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Saalam, baada ya Jumapili iliyopita timu hizo kutoka sare ya bao 1-1 ugenini.

Tayari kikosi cha Yanga kimeingia kambini jana, kujiandaa na michezo hiyo iliyopo mbele yao wakianza na Kombe la ASFC dhidi ya Tanzania Prisons.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema kikosi chao kipo tayari kwa ajili ya kwenda kutetea taji la ubingwa wa Kombe la ASFC kwa kuwakabili 'Wajelajela' hao.

Alisema dhamira kubwa ya Yanga ni kuhakikisha wanafanikiwa kutetea mataji yao yote, baada ya kuwa na uhakika wa Ligi Kuu Tanzania Bara na sasa wanalihitaji Kombe la ASFC.

"Mchezo wetu huo wa Tanzania Prisons na mingine ya Ligi Kuu tutautumia Uwanja wa Azam Complex, kutokana na Benjamin Mkapa kuwa kwenye ukarabati.

"Kuhusu mechi yetu ya kimataifa ya Jumatano ijayo, tutacheza katika Uwanja wa Mkapa na hii mechi tumekabidhi kwa mashabiki na wanachama ili kuhakikisha wanajitokeza uwanjani kwa wingi," alisema Kamwe.

Alisema mechi yao dhidi ya Tanzania Prisons mbali na kutaka ushindi katika mchezo huo, lakini wanatumia kwa ajili ya maandalizi kuelekea mechi ya marudiano dhidi ya Real Bamako kuhakikisha wanapata pointi tatu.

Kamwe alisema mipango yao ni kuvuna pointi sita katika michezo ya kimataifa ambayo watacheza nyumbani ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu kucheza robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Michuano ya kimataifa tupo nafasi ya pili katika Kundi D tukiwa na pointi nne, ukipiga hesabu vizuri tiketi ya kucheza robo fainali imenyooka kwa asilimia 90 zinategemea pointi sita katika Uwanja wa Mkapa.

"Real Bamako kurudiana nao Uwanja wa Mkapa, tunaenda kutumia vizuri kupata ushindi katika mchezo huo pamoja kusaka alama zingine tatu za US Monastir jumla itakuwa 10, ambazo zitatufanya kufuzu na kucheza hatua inayofuata," alisema Kamwe.

## KILI MARATHONI...




Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya NMB wakishiriki mbio za Km. 21 za Kill Marathon 2023, zilizoanzia na kuishia katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika, Moshi mkoani Kilimanjaro, mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa, Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Mkuranga, Peter Msaki (kushoto) na katikati ni Ofisa Ugavi wa Benki ya NMB, Linus Silayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Timu za majeshi, halmashauri hoi Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

TIMU zinazomilikiwa na majeshi, pamoja na halmashauri ambazo zinashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ziko kwenye wakati mgumu wa kujinasua na hatari ya kushuka daraja.

Timu hizo, Dodoma Jiji, KMC, Prisons, Polisi Tanzania na Ruvu Shooting kwa sasa zinapigania uhai wao wa kubaki Ligi Kuu, zikiwa kwenye nafasi tano za chini katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha jumla ya miamba 16, Yanga ikiwa kileleni ikifuatiwa na Simba.

Bodi ya Ligi imetoa orodha ya timu tano zilizo chini ya msimamo, ambapo sasa zinatakiwa kufanya kazi ya ziada kuhakikisha zinafanya vema kwenye mechi zao sita zilizobaki ili kujinusuru moja kwa moja na janga hilo, au kwenda kwenye mchujo 'play off.'

Timu pekee ya halmashauri ambayo haipo kwenye hatari ya kushuka daraja msimu huu ni Geita Gold FC inayomilikiwa na Halmashauri ya Mji wa Geita inayoshika nafasi ya tano kwa pointi 34, huku inayomilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Mbeya City, ikiwa nayo haina uhakika wa kubaki kwani inashika nafasi ya 10 kwa pointi 27 na kutakiwa kupambana sana ili kujinusuru.

Ruvu Shooting ambayo inamilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa mkoani Pwani, maeneo ya Ruvu inaburuza mkia ikiwa na pointi 17 kwenye nafasi ya 16, juu yake nafasi ya 15 ipo Polisi Tanzania, inayomikiliwa na Jeshi la Polisi Tanzania, ikiwa na alama zake 19.

Kwenye nafasi ya 14, ipo timu inayomilikiwa na Jeshi la Magereza Tanzania, Prisons ambayo nayo iko hoi bin taaban ikiwa na pointi zake 22, KMC inayomilikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inashika nafasi ya 13, ikikusanya pointi 23.

Timu nyingine iliyopo katika hali mbaya ni Dodoma Jiji FC ambayo inamilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, ina pointi 24 kwenye nafasi ya 12.

## Uhamiaji FC kiboko ya KMKM, Malindi

**Na Hawa Abdallah, Zanzibar**

TIMU ya Uhamiaji FC imerudi kwa kasi katika Ligi Kuu ya Zanzibar na kufanikiwa kuwafunga vigogo wa ligi hiyo, KMKM na Malindi.

Uhamiaji FC imeibuka na jumla ya alama sita katika michezo yake hiyo miwili ya mzunguko wa 21 na 22, hivyo kurejesha hamasa kwa mashabiki wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdi Salehe, alisema amekiimarisha kikosi chake ili kuhakikisha katika michezo hii ya mwisho wanafanya vizuri na kumaliza ligi katika nafasi nzuri.

Alisema kushinda michezo miwili mfululizo dhidi ya timu hizo kongwe katika soka la Zanzibar, kumemjengea matumaini ya kufanya vizuri hata kwenye michezo iliyobaki ili kutimiza lengo lao la kumaliza katika nafasi nne za juu.

Alisema anajua katika michezo iliyobaki itakuwa migumu zaidi kwa kuwa timu zinazogombania ubingwa zinahitaji kushinda ili kuhakikisha zinatimiza kiu yao huku na wao wakiendeleza mipango yao ya kuzoa alama katika michezo hiyo.

## Riadha A. Mashariki sasa kwa Mkapa

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Riadha ya Vijana wa Afrika Mashariki na Kati wenye umri chini ya miaka 18-20, yaliyokuwa yafanyike nchini Rwanda sasa yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi Machi 10-11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mkapa, Dar es Salaam.

Mashindano hayo yameahirishwa kufanyika nchini humo kutokana na kuwapo kwa changamoto mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Msaidizi wa Chama cha Riadha Mkoa wa Dar es Salaam (DAA), Filex Chunga, alisema maandalizi yanaendelea vema kuelekea kwenye michuano hiyo.

"Sisi kama mkoa, tutahakikisha mashindano hayo yanafanyika kama yalivyopangwa, tunaomba wadau mbalimbali wajitokeze kuona vipaji vya vijana wetu," alisema Chunga.

Katibu huyo alizitaja baadhi ya nchi ambazo zitashiriki kuwa ni wenyeji wa mashindano Tanzania, Kenya, Uganda, Sudani, Ethiopia pamoja na Eritrea.

Alisema timu hizo zitaanza kuripoti nchini kuanzia Machi 8, mwaka huu, na kwamba kwa upande wa timu ya Tanzania wachezaji wanaendelea kujifua chini ya Kocha Mkuu, Idd Muhunzi.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**TEN HAG KUSAJILI WAWILI**
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, anataka kusajili angalau wachezaji wawili muhimu msimu huu wa majira ya joto, huku mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, 24, na kiungo mshambuliaji wa Ajax Mghana Mohammed Kudus, mwenye umri wa miaka 22, wakiwa miongoni mwa malengo yake. ***(Manchester Evening News)***

**DE JONG ALENGWA UNITED**
KIUNGO wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 25, pia anasalia kulengwa na Manchester United msimu huu wa joto. ***(Sport)***

**KOVACIC AWANIWA CITY**
KLABU ya Manchester City inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Croatia, Mateo Kovacic, msimu huu wa majira ya joto, wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, atakuwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Chelsea. ***(Telegraph)***

**CHILWELL KUNG'OLEWA CHELSEA**
MLINZI wa Chelsea, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 26, ni mchezaji mwingine anayelengwa na Manchester City msimu ujao. ***(Football Insider)***

**ROQUE AITAKA ARSENAL**
MSHAMBULIAJI wa Athletico Paranaense raia wa Brazil, Vitor Roque, amesema yuko tayari kujiunga na Barcelona, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, kunyatiwa na Arsenal. ***(Sport)***

**KEITA KUREJESHWA UJERUMANI**
KLABU ya Borussia Dortmund na klabu ya zamani ya Naby Keita ya RB Leipzig zina nia ya kumsajili kiungo huyo wa kati wa Guinea mwenye umri wa miaka 28, mkataba wake na Liverpool utakapokamilika msimu huu. ***(Bild)***

**SOYUNCU HUYOOO ATLETICO**
KLABU ya Atletico Madrid imekubaliana na beki wa Uturuki, Caglar Soyuncu, mwenye umri wa miaka 26, juu ya uhamisho wa bila malipo mkataba wake Leicester City utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(90 Min)***

**JUDE AMULIKWA MADRID**
REAL Madrid msimu huu wa majira ya joto, wanamulika Jude Bellingham na beki wa RB Leipzig, Croatia Josko Gvardiol, 21. ***(Sport)***

**KANTE KUBAKI CHELSEA**
MCHEZAJI N'Golo Kante alikuwa na chaguo la kuondoka Chelsea kwa uhamisho wa bila malipo msimu huu, lakini kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 31, anataka kubakia Stamford Bridge na anakaribia kuafiki mkataba mpya. ***(Fabrizio Romano)***

**MAATSEN BADO YUPO SANA**
KLABU ya Burnley inataka kumbakisha beki wa kulia wa Uholanzi, Ian Maatsen mwenye umri wa miaka 20, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo kutoka Chelsea, Turf Moor msimu ujao. ***(Sun)***

**PATTERSON AJIWEKA TAYARI**
GOLIKIPA wa Sunderland, Anthony Patterson, mwenye umri wa miaka 22, yuko tayari kuitwa kwa kikosi cha Gareth Southgate cha England kwa ajili ya kufuzu kwa Euro 2024 mwezi ujao. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: MAN CITY WASAHAU MATAJI MA3

**Sahau, unapoanza kuzungumzia hilo, hatuko tayari na hakuna hata sekunde moja kufikiria hilo...**

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amepuuzilia mbali uwezekano wa Manchester City kutwaa mataji matatu msimu huu, akisema wachezaji wake lazima "wasahau kuhusu hilo" baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Bristol City inayoshiriki michuano ya chini na kujihakikishia nafasi ya kutinga robo fainali ya Kombe la FA.

Mabao mawili kutoka kwa Phil Foden na mkwaju wa kipindi cha pili kutoka kwa Kevin De Bruyne yalihitimisha ushindi na kuiweka City kwenye njia ya mafanikio katika mashindano matatu - Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA.

Lakini Guardiola, ambaye aliiongoza Barcelona kushinda mataji matatu ya ligi, Kombe na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2009, alisema kufikiria marudio hayo hapo City ni ngumu.

"Hapana, sahau kuhusu hilo (mataji matatu)," alisema Guardiola

"Sahau, unapoanza kuzungumzia hilo, unaanza kupoteza mashindano na kuacha mashindano.

"Hatuko tayari. Hakuna hata sekunde moja kufikiria hilo, tunafikiria tu kuhusu mchezo unaofuata dhidi ya Newcastle.

"Jambo pekee nililosema mara nyingi - nimekerwa kulisema tena na tena na tena baada ya kile kilichotokea katika miaka iliyopita.

"Hili ndilo taji kubwa zaidi. Hili ndilo taji kubwa zaidi. Kubwa zaidi. Najua hatuwezi kuangusha pointi kwenye Ligi Kuu kwa sababu tuna timu juu yetu (Arsenal) na (Manchester) United ipo nyuma yetu.

"Na Ligi ya Mabingwa Ulaya, tunaona kitakachotokea katika wiki mbili. Cha muhimu ni kwamba tupo, lakini bila shaka, tutaendelea kwa muda mrefu iwezekanavyo."

Man City ipo nyuma ya vinara wa Ligi Kuu England, Arsenal kwa pointi mbili, wakiwa wamecheza mechi moja zaidi, na wametoka sare ya bao 1-1 katika mechi ya mkondo wa pili wa hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya RB Leipzig.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,083,8

MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT.0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KANTE AKARIBIA KUSAINI MKATABA MPYA



**LONDON, England**

KIUNGO N'Golo Kante anakaribia kukubali kusaini mkataba mpya na Chelsea, vyanzo vimeiambia ESPN.

Kiungo huyo mkataba wake unamalizika Juni mwaka huu, lakini mazungumzo yamekwenda vizuri na pande hizo mbili zinakamilisha maelezo ya mkataba mpya wa miaka mitatu ambao utaendelea hadi Juni 2026.

Kante alitaka kusalia Chelsea muda wote, huku vyanzo vikisema ana furaha katika klabu hiyo licha ya matatizo ya jeraha aliyokabiliana nayo kwa miaka miwili iliyopita.

Kocha aliyekalia kuti kavu, Graham Potter na wamiliki wapya pia walikuwa na nia ya kumbakisha na majadiliano yalipata mafanikio mwishoni mwa Januari.

Potter anamwona mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa kama msaidizi mzuri katika usajili wa Januari wa Enzo Fernandez katika safu ya kati, eneo ambalo Chelsea imekuwa na shida msimu wote hadi sasa.

Kante alihamia Stamford Bridge kutoka Leicester City msimu wa majira ya joto wa 2016 na ameshinda Ligi Kuu England, Ligi ya Europa na Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati akiwa na klabu hiyo.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amekuwa nje ya uwanja kutokana na majeraha tangu Agosti, hivyo kumaanisha kwamba alikosa pia michuano ya Kombe la Dunia.

Lakini sasa anafanya mazoezi na kikosi hicho na yuko tayari kurejea kwenye kikosi cha kwanza.

Potter pia atakaribisha kurejea kwa Kante katika kikosi chake kilichokumbwa na majeraha baada ya Jumanne kujua kwamba Thiago Silva atakuwa nje kwa wiki sita kutokana na majeraha ya goti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anaungana na Christian Pulisic, Cesar Azpilicueta, Edouard Mendy na Armando Broja kwenye orodha ya majeruhi.

'The Blues' waliopo nafasi ya 10 watacheza na Leeds United walio katika hatari ya kushuka daraja Jumamosi katika Uwanja wa Stamford Bridge, kabla ya kuwakaribisha Borussia Dortmund wiki ijayo katika mechi ya mkondo wa pili wa hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kupoteza kwa bao 1- 0 nchini Ujerumani.

# Diaz kuikosa Real Madrid

**LIVERPOOL, England**

LUIS Diaz hatakuwa fiti kwa wakati katika mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ya Liverpool ugenini dhidi ya Real Madrid, kocha Jurgen Klopp amethibitisha.

Diaz hajawachezea 'Wekundu' hao tangu alipoumia goti katika mechi ya Ligi Kuu England wakati wakipoteza kwa mabao 3-2 dhidi ya Arsenal Oktoba mwaka jana.

Katika mahojiano na Sky Sports wiki mbili zilizopita, mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia alionekana kudokeza kuwa huenda mechi ya mkondo wa 16-bora itakayopigwa Machi 15, mwaka huu ndiyo atarejea, akisema: "Tusubiri kidogo tuone ni lini nitarejea uwanjani na kama ni (Santiago) Bernabeu, haitakuwa tatizo."



Lakini Klopp alifichua kuwa winga huyo bado hajarejea mazoezini na atakosa mechi hiyo muhimu, huku Liverpool wakitarajia kujiondoa katika hali ambayo haikufikiriwa baada ya kuchapwa mabao 5-2 na Madrid katika mechi ya kwanza iliyochezwa Anfield wiki iliyopita.

Licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, kukosekana kwa muda mrefu, Klopp ana imani kuwa anaweza kuwa na ushawishi mkubwa kwenye timu atakaporejea, na kuongeza kwa waandishi wa habari: "Inakadiriwa kuwa labda wiki ijayo atakuwa anajifua na timu.

"Nina maoni chanya juu yake kwamba kuna nafasi nzuri ya kuwa na mchango kwenye mechi. Tutaona ni muda gani itachukua.

"Atakaporudi, atakuwa mzuri sana na mwenye kiwango bila shaka. Hiyo ni wazi. Ni haraka gani, sijui. Lazima tuone."

**HABARI MICHEZO**

326,057/-

# PHIRI, MZIZE, WAMTAFUTIA KASI SIMCHIMBA FA CUP

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mechi za Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) maarufu Kombe la FA, zikitarajiwa kuchezwa leo hatua ya 16-bora, straika wa Simba, Moses Phiri na wa Yanga, Clement Mzize, wanakabana koo katika mbio za ufungaji bora kila mmoja akiwa amepachika mabao manne.

Kwa mujibu wa takwimu za michuano hiyo, Phiri na Mzize wanakamata nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji wakiwa na idadi hiyo ya mabao, huku kinara wa kucheka na nyavu kwenye michuano hiyo akiwa ni Andrew Simchimba wa Ihefu FC atupia mpira kimyani mara tano hadi sasa.

Mbali na mastraika hao wa Simba na Yanga, wengine ambao wana mabao manne mpaka sasa ni Richardson Ng'ondya na Sadala Lipangile wa KMC.

Hata hivyo, kinara wa mabao, Simchimba, Phiri, Mzize na Sadala, wana uwezo wa kuendelea kuongeza idadi hiyo na kupambana kuwania ufungaji bora kwa sababu timu zao bado zipo kwenye michuano hiyo.

Takwimu za michuano hiyo zinaonyesha kuwa wachezaji waliofunga mabao matatu ni Lucas Daud wa Buhaya FC, Jacob Peter wa Polisi Katavi, Salum Bosco wa Magereza Dar, na Ismail Mgunda wa Tanzania Prisons.

Kati ya hawa ni Mgunda tu ndiye anayeweza kuongeza idadi yake ya mabao kwa sababu timu yake ya Prisons bado ipo, zingine zikiwa zimetolewa.

Ratiba ya michuano hiyo ya Kombe la FA inaonyesha kuwa baada ya Simba kucheza leo dhidi ya African Sports kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, kesho Yanga itacheza dhidi Prisons kwenye Uwanja Azam Complex, Chamazi, wakati Jumamosi Ihefu itakipiga dhidi ya Pan African kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya.

Mtibwa Sugar itakuwa nyumbani, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro ikiikaribisha KMC FC wakati Singida Big Stars itacheza dhidi ya JKT Tanzania, katika Uwanja wa Liti mkoani Singida.

Hatua hiyo ya 16-bora ya FA itamalizika Jumapili kwa michezo miwili, ambapo Azam itakuwa nyumbani Chamazi Uwanja wa Azam Complex kucheza dhidi ya Mapinduzi FC ya Mwanza huku siku hiyo hiyo Kagera Sugar ikiialika Mbeya City kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

# YANGA SC YATIKISA

INATOKA UK. 24



Mzize

Kwenye mechi za ushindi wa nyumbani, Yanga imeshinda mechi 10 kati ya 12 ilizocheza, na michezo miwili ambayo ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Azam na 1-1 dhidi ya Simba.

Timu ya Azam inashika nafasi ya pili kwa kushinda mechi nyingi za nyumbani ambayo nayo kama Yanga imeshinda mechi 10 kati ya 12, lakini Wanalambalamba hao wako kwenye nafasi ya pili kwa sababu mechi zao mbili moja wamepoteza, tofauti ya wenzao ambao wametoka sare zote.

Azam ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Geita Gold nyumbani na kuchapwa mabao 3-2 dhidi ya Yanga.

Simba iko kwenye nafasi ya tatu kwa kwa kushinda mechi tisa nyumbani kati ya 11 ilizocheza huku Singida Big Stars ikiwa nafasi ya nne kwa kucheza mechi 12, ikishinda tisa.

Mabingwa watetezi, Yanga wanaongoza kwa kushinda mechi nyingi, ikifanya hivyo mara 20, ikifuatiwa na Simba mara 16, ikitoa sare mara mbili tu ambayo ni idadi ya chini zaidi kuliko timu yoyote, ikiruhusu mabao machache zaidi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, ambayo ni 10, ikifuatiwa na Simba iliyoruhusu wavu wake kutikiswa mara 14.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/03/23 | 20:30 | Southampton FC vs Leicester City | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 02. 04/03/23 | 20:30 | Tenerife CD vs SD Eibar | 2.36 | 2.80 | 3.40 |
| 03. 04/03/23 | 20:45 | FC Volendam vs FC Emmen | 2.60 | 3.35 | 2.60 |
| 04. 04/03/23 | 22:45 | ACF Fiorentina vs AC Milan | 2.80 | 3.20 | 2.48 |
| 05. 04/03/23 | 22:45 | Standard Liege vs KVC Westerlo | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 06. 04/03/23 | 23:00 | CD Mirandes vs Real Oviedo | 2.48 | 2.90 | 3.15 |
| 07. 05/03/23 | 14:30 | Spezia Calcio vs Hellas Verona | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 08. 05/03/23 | 15:30 | Hansa Rostock vs Karlsruher SC | 2.70 | 3.30 | 2.50 |
| 09. 05/03/23 | 16:00 | Real Valladolid vs Espanyol Barcelona | 2.24 | 3.15 | 3.25 |
| 10. 05/03/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Everton FC | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 11. 05/03/23 | 19:30 | Liverpool FC vs Manchester United | 2.38 | 3.40 | 2.80 |
| 12. 05/03/23 | 19:30 | VfL Wolfsburg vs Eintracht Frankfurt | 2.43 | 3.40 | 2.75 |
| 13. 05/03/23 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Athletic Bilbao | 2.90 | 3.00 | 2.55 |
| 14. 05/03/23 | 21:00 | Santa Clara Azores vs Vitoria SC Guimaraes | 2.70 | 3.15 | 2.60 |
| 15. 05/03/23 | 22:00 | SC Cambuur vs Go Ahead Eagles | 2.75 | 3.30 | 2.47 |
| 16. 05/03/23 | 22:45 | AS Roma vs Juventus Turin | 2.37 | 3.05 | 3.10 |
| 17. 05/03/23 | 22:45 | Stade Rennes vs Olympique Marseille | 2.75 | 3.35 | 2.45 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 02/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1292 | South Korea U20 vs Oman | 1.34 | 4.68 | 7.08 |
| 15:00 | 2278 | CA Central Cordoba SE Reserve vs CA Platense | 3.21 | 3.00 | 2.20 |
| 15:00 | 2964 | Velez Sarsfield Reserve vs CA Talleres de Cordoba Reserve | 1.66 | 3.54 | 4.69 |
| 15:00 | 3175 | Tajikistan U20 vs Jordan | 3.06 | 3.43 | 2.08 |
| 15:00 | 3313 | Argentinos Juniors Reserve vs CA Tigre Reserve | 1.69 | 3.42 | 4.66 |
| 15:15 | 2154 | Kuching FA vs Selangor FC | 2.77 | 3.38 | 2.21 |
| 16:00 | 1278 | Simba vs African Sports | 1.03 | 7.50 | 15.00 |
| 16:00 | 1414 | FK Radnicki 1923 vs Backa Topola | 3.07 | 3.02 | 2.20 |
| 16:00 | 1518 | Pahang FA vs Kelantan FA | 1.77 | 3.49 | 3.85 |
| 16:00 | 2584 | Al Fateh (KSA) vs AL Tai | 1.80 | 3.30 | 3.50 |
| 16:00 | 2628 | NK Ilirija vs NK Nafta | 2.56 | 3.24 | 2.44 |
| 16:00 | 4110 | Hadiya Hosahina FC vs Mekelakeya | 2.37 | 2.80 | 3.11 |
| 16:00 | 5193 | AL Faiha vs Abha | 1.96 | 3.20 | 3.10 |
| 16:30 | 1180 | Tiddim Road Athlectic Club vs Gokulam Kerala FC | 2.81 | 3.17 | 2.28 |
| 16:30 | 1571 | AL Bataeh (UAE) vs AL Khaleej Khor Fakkan | 2.88 | 3.44 | 2.12 |
| 16:30 | 2197 | US Monastir vs US Tataouine | 1.52 | 3.18 | 7.38 |
| 16:30 | 5600 | Al Ain vs Dibba Al Fujairah | 1.16 | 6.18 | 11.32 |
| 16:30 | 5611 | US Ben Guerdane vs Esperance Tunis | 4.71 | 3.12 | 1.73 |
| 16:55 | 2273 | Al-Shamal vs Qatar SC | 3.13 | 3.49 | 1.98 |
| 16:55 | 5031 | Al Rayyan SC vs Umm-Salal SC | 2.17 | 2.91 | 3.27 |
| 17:00 | 3275 | Mosaset AL Bireh vs Markez Balata | 3.39 | 3.34 | 1.94 |
| 17:00 | 4289 | AL Sahel vs Al Fehaheel | 2.62 | 3.13 | 2.45 |
| 17:00 | 5662 | Senegal U20 vs Benin | 1.47 | 3.57 | 7.23 |
| 18:00 | 3546 | Nea Salamis vs AEL Limassol | 2.51 | 2.96 | 2.75 |
| 18:00 | 4362 | Islami Qalqilya vs Shabab Al Dhahiriya | 11.30 | 5.96 | 1.17 |
| 18:00 | 5646 | CFR Cluj vs UTA Arad | 1.42 | 3.98 | 7.33 |
| 18:30 | 1665 | Al Ahli Manama vs AL Khalidiyah | 3.57 | 3.16 | 1.99 |
| 18:30 | 2434 | Al Shabbab vs AL Badii | 1.56 | 3.68 | 5.39 |
| 18:30 | 2616 | ASEC Mimosas vs Bassam | 1.68 | 3.12 | 5.40 |
| 19:00 | 1790 | Arba Minch Kenema vs Wolkite City FC | 2.30 | 2.85 | 3.17 |
| 19:15 | 1770 | Baniyas vs Ajman Club | 2.15 | 3.29 | 2.93 |
| 19:15 | 3721 | Ittihad Kalba vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 4.11 | 3.49 | 1.72 |
| 19:30 | 1718 | Lekhwiya SC vs Al Arabi Doha SC | 2.06 | 3.40 | 3.04 |
| 20:00 | 1765 | Aalborg vs Viborg FF | 2.85 | 3.26 | 2.26 |
| 20:00 | 1867 | Kolubara vs Javor Ivanjica | 2.35 | 3.09 | 2.78 |
| 20:00 | 4755 | Hilal Al-Quds vs Thagafi Tulkarem | 1.29 | 4.61 | 8.41 |
| 20:00 | 4977 | Uganda vs Nigeria U20 | 3.21 | 2.79 | 2.33 |
| 20:30 | 2152 | Al Wehda vs Al Hilal Riyadh | 6.64 | 4.39 | 1.45 |
| 20:45 | 1041 | PSV Eindhoven vs ADO Den Haag | 1.14 | 6.82 | 13.44 |
| 21:00 | 2907 | Gremio RS U20 vs Atletico PR U20 | 2.22 | 3.05 | 2.75 |
| 21:00 | 3930 | Anorthosis Famagusta vs Olympiakos Nicosia | 1.81 | 3.27 | 4.15 |
| 21:00 | 4375 | Steaua Bucuresti vs Petrolul Ploiesti | 1.35 | 4.39 | 8.35 |
| 21:00 | 5535 | Racing Club Dabidjan vs AF Amadou Diallo | 3.75 | 2.46 | 2.15 |
| 21:30 | 3016 | Tiradentes CE vs Pague Menos CE | 2.47 | 2.75 | 2.65 |
| 22:00 | 4283 | Debreceni VSC vs Puskas Akademia | 2.33 | 3.42 | 2.64 |
| 22:15 | 3373 | FC Rotkreuz vs Servette Geneva | 12.33 | 6.58 | 1.14 |
| 22:30 | 3604 | Juventus U23 vs Vicenza | 2.53 | 3.21 | 2.54 |
| 22:45 | 1070 | Royal Antwerp vs Union Saint Gilloise | 2.44 | 3.41 | 2.61 |
| 23:00 | 3735 | De Graafschap vs Ajax | 11.37 | 6.41 | 1.17 |
| 23:00 | 3939 | Real Madrid vs Barcelona | 1.96 | 3.35 | 3.62 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Machi 2, 2023
Nipashe



UKURASA 21

Guardiola: Man City wasahau mataji ma3

# ROBERTINHO AANIKA KIKOSI CHA FA CUP

●●●Ni kitakachoivaa African Sports Uwanja wa Uhuru leo, Kibu atupwa nje wiki moja, aitaja Vipers...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kikosi cha Simba kikitarajiwa kushuka Uwanja wa Uhuru leo kuikaribisha African Sports kutoka Tanga kwenye mchezo wa hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, Kocha Mkuu wa Wekundu wa Msimbazi hao, Robertinho Oliveira, ameweka wazi wachezaji atakaowapa nafasi leo huku akimulika zaidi mechi ijayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers FC ya Uganda.

Baada ya mchezo huo wa leo utakaopigwa saa 10:00 alasiri, Simba itaendelea na maandalizi yake ya mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers itakayopigwa Jumanne ijayo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika mchezo uliopigwa Uwanja wa St. Mary's nchini Uganda Jumamosi iliyopita, Simba ilishinda bao 1-0 shukrani kwa Henock Inonga, aliyeiwezesha kuvuna pointi tatu za kwanza baada ya michezo mitatu ya hatua hiyo ya makundi.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema wamejipanga kuhakikisha wanashinda dhidi ya African Sports ili kutinga robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam, ASFC.

Alisema siku zote malengo ya Simba ni kushinda kila taji la michuano wanayoshiriki na kwa hali hiyo wanahitaji kupata ushindi katika mchezo wa leo.

Kocha huyo raia wa Brazil, alisema leo wanategemea kuwatumia wachezaji ambao hawapati nafasi kubwa kikosini kwa kuwa wiki ijayo wana mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers.

"Tumejipanga kuhakikisha tunashinda mchezo wa kesho (leo) wa Kombe la Shirikisho dhidi ya African Sports, Simba ni timu kubwa na tunahitaji kushinda kila taji na tupo tayari.

"Tunategemea kuwatumia wachezaji ambao hawajapata nafasi kubwa kikosini kwa kuwa tuna mchezo wa marudiano nyumbani dhidi ya Vipers kwa hiyo tunaziangalia mechi zote," alisema Robertinho.

Hata hivyo, kuelekea mchezo wa leo, Robertinho atalazimika kumkosa mshambuliaji, Kibu Denis, ambaye atakuwa nje kwa wiki moja kutokana na kupata majeraha katika mchezo uliopita wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers.

**Kibu alipata maumivu ya mguu na baada ya vipimo daktari wa timu hiyo, Edwin Kagabo, amesema anahitaji kuwa nje kwa mudu wa wiki moja ili kupona kabisa, lakini Simba itaendelea kumkosa Augustine Okrah, ambaye ndiyo kwanza ameanza ma zoezi mepesi chini ya uangal izi kabla ya kujiunga pamoja na wenzake.**

"Kibu alipata maumivu katika mchezo uliopita dhidi ya Vipers, hayakuwa mabaya sana, lakini inabidi akae nje ya uwanja kwa muda wa wiki moja ili kupona kabisa," alisema Dk. Kagabo.

Kwa upande wa Kocha wa African Sports, Mussa Rashid, alisema ana waheshimu Simba lakini wamejiandaa vizuri kuonyesha ushindani mkubwa katika mchezo huo.

"Tunatambua mchezo utakuwa na ushindani mkubwa na malengo yetu makubwa yalikuwa ni kufika na kucheza hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho," alisema kocha huyo.



Clatous Chama, mmoja wa nyota wa Simba ambaye huenda akampumzishwa mechi ya leo dhidi ya African Sports kwa ajili ya kuisubiri Vipers Jumanne ijayo.

## Yanga SC yatikisa kwa rekodi Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

HUKU straika wake, Fiston Mayele, akiendelea kuongoza kwenye orodha ya wafungaji akiwa na mabao 15, timu ya Yanga imeendelea kujizolea rekodi lukuki za kufanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ambapo kwa sasa inaongoza kwa kushinda mechi nyingi ugenini na nyumbani pia.

Mbali na rekodi hiyo, Yanga iliyopo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa pointi 62, ndiyo timu iliyoshinda mechi nyingi zaidi za jumla, ikitoka sare mara chache zaidi na kufungwa mabao machache pia.

Kwa mujibu wa rekodi na takwimu za Ligi Kuu hadi kufikia raundi ya 24, Yanga imeshinda mechi 10 kati ya 11 za ugenini ikiwa na maana haijashinda mchezo mmoja tu kati ya hizo na hiyo ilikuwa ni Novemba 29, mwaka jana, ilipochapwa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu, katika Uwanja wa Highland, Estates, Mbarali mkoani Mbeya.

Simba inashika nafasi ya pili kwa timu zilizoshinda mechi nyingi ugenini, ikishinda mara saba kati ya mechi 12 ilizocheza hadi kufikia raundi hiyo.

Kwenye mechi tano ambazo imeshindwa kufanya kuibuka na ushindi nyumbani ni dhidi ya Azam FC ilipochapwa bao 1-0, sare ya bao 1-1 dhidi ya Wanalambalamba hao pia sare ya 1-1 dhidi za Mbeya City, Yanga, Kagera Sugar na nyingine kwa Singida Big Stars.

Timu ya Singida Big Stars iko kwenye nafasi ya tatu kwa timu zilizoshinda mechi nyingi ugenini, ikicheza mechi 12 na kushinda tano, Azam ipo nafasi ya nne, ikishinda nne ugenini kwa michezo yake 12, huku Namungo ikiwa nafasi ya tano, ikishinda mechi nne, lakini ikicheza mechi 14 za ugenini mpaka sasa.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >